Haliuzwi
JUNI 15, 2026
/islamicftz
Dhul-Hijja 29 1447
IMAAN
ISSN 5618 - NO. 588
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

Hasara ilioje kupuuza ibada kisa Kombe la Dunia



# Bajeti zadhihirisha fursa, vikwazo sekta fedha za Kiislamu



Waislamu Uganda wadai mashujaa wao watambuliwe katika historia ya taifa



## DCEA YAONYA WANANCHI: "Nibebee kifurushi hiki" kunaweza kuwa ni mtego wa kukupeleka jela

## Rais Dkt. Mwinyi atangaza siku ya mapumziko Z'bar

- Mufti Zubeir amtaka Mwinyi kumshawishi Rais Samia mapumziko yawe Tanzania nzima

## Matibabu ya macho bure yavutia mamia Morogoro

- Wenye changamoto wapata miwani, dawa
- 250 kufanyiwa upasuaji



Misikiti irudi kuwa vituo vya kuutumikia umma

Fitch: Ukwasi wa Sukuk waanza kuimarika baada ya vita vya Iran

NA MWANDISHI WETU



# Mwaka Mpya wa Hijria: Rais Mwinyi atangaza siku ya mapumziko Zanzibar

## Mufti Zubeir aibua hoja ya mapumziko ya Hijriya nchi nzima

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Hussein Mwinyi, ametangaza Jumatano Juni 17, 2026 kuwa siku ya mapumziko rasmi kwa ajili ya kuukaribisha Mwaka Mpya wa Kiislamu 1448 Hijria.

Tamko hilo limetolewa leo Jumatatu Juni 15, 2026 katika Ikulu Zanzibar, na kutolewa kwa umma kupitia taarifa ya Kaimu Mkurugenzi Mawasiliano ya Rais Ikulu, Raqey Mohamed.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hatua ya kutenga siku hiyo kuwa ya mapumziko ni utekelezaji wa uamuzi wa Serikali ya Zanzibar wa kuutambua Mwaka Mpya wa Kiislamu kuwa miongoni mwa siku muhimu zinazostahili kupewa nafasi maalumu katika jamii.

Rais Mwinyi amesema siku hiyo itakuwa fursa kwa wananchi, hususan waumini wa dini ya Kiislamu, kuukaribisha mwaka mpya kwa kufanya ibada, dua na matendo mema, huku wakimuomba Mwenyezi Mungu kuendelea kuijaalia Zanzibar na Tanzania kwa ujumla amani, umoja na ustawi.

" Siku hiyo itatoa fursa kwa wananchi hususani waumini wa dini ya Kiislamu kuukaribisha mwaka mpya kwa ibada, dua, na matendo mema pamoja na kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kujaalia Zanzibar na Tanzania kwa ujumla amani, umoja na ustawi," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Katika kuukaribisha mwaka mpya wa Hijria, Rais Mwinyi amewataka wananchi kutumia kipindi hicho kama nafasi ya kujitathmini kuhusu mwenendo wao wa maisha, kuimarisha uchaMungu na kuendeleza maadili mema yenye kujenga familia na jamii yenye mshikamano.

Aidha, amewahimiza wananchi kuendelea kushirikiana, kusaidiana na kudumisha misingi ya upendo na mshikamano ambao ni nguzo muhimu katika kujenga taifa lenye amani na maendeleo endelevu.

Mwaka Mpya wa Kiislamu huanza baada ya kuonekana kwa mwezi wa Muharram, ambao ni mwezi wa kwanza katika kalenda ya Hijria. Kalenda hiyo hutumika na Waislamu duniani kote kufuatilia matukio mbalimbali ya kidini, yakiwemo ibada na kumbukumbu muhimu.

Kutangazwa kwa siku ya mapumziko kunatarajiwa kuwapa wananchi nafasi ya kushiriki shughuli za kidini na kijamii bila vikwazo vya majukumu ya kawaida ya kila siku.

Serikali ya Zanzibar imekuwa ikisisitiza umuhimu wa kuhifadhi maadili, kuimarisha mshikamano wa kijamii na kutoa nafasi kwa wananchi kushiriki katika matukio yenye umuhimu wa kidini na kitaifa.

Kwa hatua hiyo, wananchi wa Zanzibar wataungana na Waislamu wengine duniani kuanza mwaka 1448 Hijria wakiwa na matumaini mapya, dua za amani na azma ya kuendelea kujenga jamii yenye maadili na umoja.



### Mufti aibua hoja ya mapumziko ya Hijriya nchi nzima

Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Dkt. Abubakari Zubeir Ally amemuomba Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Mwinyi kumshawishi Rais wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ili mapumziko ya Mwaka Mpya wa Kiislamu Hijiryya yawe Nchi nzima.

Mufti ameyasema hayo Juni 15, 2026 mbele ya Rais Dkt. Mwinyi wakati wa mwendelezo wa Maadhimisho ya Mwaka Mpya wa Kiislamu visiwani Zanzibar.

"Mimi nitumie nafasi hii kwamba mapumzo tunayaomba pia na kule Bara yaenee kwasababu Nchi ni moja, hii inaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaomba na sisi ieneee Tanzania nzima kwa kuwa Dkt. Mwinyi amethubutu kufanya jambo hili, namuomba Mungu awape zaidi Taufiq na uweze kumshauri Rais wa Jamhuri hili jambo liweze kuzagaa na kwa jambo hili ni sababu ya moja kwa moja kupata daraja la juu katika pepo,"amesema Mufti Zubeir.




HABARI DODOMA

NA MWANDISHI WETU

# Bajeti 2026/27 zadhihirisha fursa, vikwazo sekta fedha za Kiislamu

- Uganda, Kenya zatambua Sukuk
- Wadau wasema walitegemea mageuzi ya kodi

Bajeti za mwaka 2026/27 katika nchi za Afrika Mashariki zimeonesha mwelekeo tofauti kuhusu nafasi ya huduma ya fedha za Kiislamu katika uchumi, huku Kenya na Uganda zikianza kuangalia Sukuk kama chanzo mbadala cha fedha za maendeleo, Zanzibar ikiendelea kunufaika na mfumo huo, na Tanzania Bara ikikabiliwa na wito wa kufanya mageuzi ya kodi ili kuharakisha ukuaji wa sekta hiyo.

Wakati mahitaji ya fedha za kugharamia miradi ya maendeleo yakiendelea kuongezeka na madeni ya umma yakizidi kuwa changamoto kwa nchi nyingi, serikali mbalimbali katika ukanda huo zimeanza kutafuta mbinu mpya za kuvutia mitaji na kupanua ushiriki wa wananchi katika mifumo rasmi ya kifedha.

## Kenya yafikiria Sukuk kuziba nakisi ya bajeti

Nchini Kenya, Serikali imeweka wazi kwa mara ya kwanza katika bajeti yake kwamba inafikiria kutumia Sukuk kama sehemu ya mkakati wa kufadhili matumizi ya umma na kupunguza utegemezi wa mbinu za kawaida za ukopaji.

Akiwasilisha bajeti ya mwaka 2026/27, Waziri wa Hazina wa Kenya, John Mbadi, alisema Serikali inafikiria kuanzisha Sukuk ili kuwezesha upatikanaji wa ukwasi kutoka masoko ya fedha za Kiislamu.

Hatua hiyo inakuja wakati Kenya ikikabiliwa na nakisi ya bajeti inayokadiriwa kufikia takribani Shilingi trilioni 1.2 za Kenya, hali inayolazimu Serikali kutafuta vyanzo vipya vya fedha.

Kwa mujibu wa Mbadi, Sukuk zitasaidia kupanua wigo wa wawekezaji kwa kuvutia taasisi na mifuko ya uwekezaji inayopendelea bidhaa za kifedha zinazozingatia misingi ya Sharia. Serikali pia inaamini hatua hiyo itasaidia kukuza ujumuishi wa kifedha na kuimarisha masoko ya mitaji ya ndani na ya kimataifa.

Iwapo mpango huo utatekelezwa, Kenya itaungana na nchi kadhaa za Afrika ambazo tayari zimefanikiwa kutumia Sukuk kufadhili miradi ya maendeleo na miundombinu.

## Uganda yaingiza Sukuk katika mkakati wa ufadhili wa bajeti

Nchini Uganda, Sukuk pia imepewa nafasi katika mkakati wa Serikali wa kupata fedha za kutekeleza vipaumbele vya maendeleo.

Akiwasilisha bajeti ya mwaka 2026/27, Waziri wa Fedha wa Uganda, Matia Kasaija, alisema Serikali inakusudia kupanua vyanzo mbadala vya fedha ili kuongeza nafasi ya kifedha kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo huku ikiendelea kulinda uhimilivu wa deni la taifa.

"Kupanua vyanzo mbadala vya fedha, ikiwemo ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP), mitaji ya ubia (venture capital), nyenzo bunifu za kifedha kama Sukuk, pamoja na kuorodhesha mashirika ya umma yenye uwezo wa kibiashara katika soko la hisa," alisema Kasaija akieleza mkakati wa kugharamia bajeti ya mwaka ujao.

Kauli hiyo imekuja wakati Uganda ikiendelea na maandalizi ya kutoa Sukuk yake ya kwanza ya Serikali.

Wachambuzi wa uchumi wanaamini hatua hiyo inaweza kuisaidia nchi hiyo kuvutia wawekezaji wapya kutoka ndani na nje ya nchi, hususan wale wanaotafuta bidhaa za kifedha zinazokubalika kwa mujibu wa Sharia.

## Zanzibar yaendelea kuvuna matunda ya Sukuk

Tofauti na Kenya na Uganda ambazo bado ziko katika hatua za maandalizi, Zanzibar tayari imekuwa ikitumia Sukuk kufadhili miradi ya maendeleo kwa miaka kadhaa.

Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaonyesha kuwa Serikali imeendelea kutenga Sh6.5 bilioni kila mwezi kwa ajili ya kulipa mtaji na faida za wawekezaji wa Sukuk kupitia Mfuko wa Miundombinu.

Hadi Machi 2026, Serikali ilikuwa imetenga jumla ya Sh59.58 bilioni kwa ajili ya kulipa mtaji na faida za wawekezaji wa Sukuk. Katika kipindi hicho wawekezaji walikuwa wamepokea Sh13.03 bilioni kama nusu ya faida ya mwaka, huku malipo ya nusu ya pili yaliyofanyika Aprili 2026 yakifanya jumla ya faida zilizolipwa kufikia Sh26.06 bilioni.

Serikali ilisema ilianzisha Sukuk kama mfumo mbadala wa uwekezaji unaozingatia misingi ya Sharia ili kupanua vyanzo vya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Fedha zilizopatikana kupitia Sukuk zimetumika kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Terminal II ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Bandari ya Mangapwani, Soko la Samaki Mkoani, Soko la Samaki Fungurefu pamoja na miradi ya barabara katika Unguja na Pemba.

Wadau wa sekta hiyo wanaeleza kuwa uzoefu wa Zanzibar unaonyesha kuwa Sukuk inaweza kuwa nyenzo muhimu ya kugharamia maendeleo bila kutegemea mikopo ya kawaida pekee.

## Tanzania yakosolewa kwa kutokuweka mageuzi ya kodi

Wakati nchi jirani zikianza kuingiza Sukuk katika mikakati yao ya ufadhili wa maendeleo, wataalamu wa fedha za Kiislamu wanasema bajeti za Tanzania Bara na Zanzibar bado hazijaweka hatua mahsusi za kodi zinazoweza kuharakisha ukuaji wa sekta hiyo.

Uchambuzi wa kampuni ya Siraat Shariah Audit and Advisory unaonyesha kuwa Tanzania Bara imeruhusu utoaji wa huduma za benki zisizo na riba kupitia Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha za mwaka 2025, lakini haijatumia mfumo huo kama chombo cha ufadhili wa Serikali.

Ripoti hiyo pia inaeleza kuwa sheria za kodi bado zimejengwa zaidi katika mfumo wa fedha unaotegemea riba na hazitoi utambuzi wa moja kwa moja kwa bidhaa za fedha za Kiislamu kama Murabaha, Ijara, Sukuk na Takaful.

Kwa mujibu wa wataalamu hao, hali hiyo inaweza kufanya baadhi ya miamala ya fedha za Kiislamu kubeba gharama kubwa zaidi za kodi ikilinganishwa na bidhaa za kawaida za kifedha.

**HABARI**
**MOROGORO**

NA MWANDISHI WETU

# Matibabu ya macho bure yavutia mamia Morogoro

- Wenye changamoto wapata miwani, dawa
- 250 kufanyiwa upasuaji




Mamia ya wananchi wa mkoa wa Morogoro wamepata fursa ya kufanyiwa uchunguzi wa afya ya macho na kisha kwa wale wenye matatizo kutibiwa bure kupitia kambi maalumu iliyoanza Juni 15 hadi 18.

Matibabu hayo yaliyoandaliwa na taasisi ya The Islamic Foundation kwa ufadhili wa Mercy Outreach Global yanafanyika katika kituo cha Al-Jamih for Mother and Child Health Care kilichopo Msamvu, karibu na Ofisi za Uhamiaji, Morogoro.

Huduma hizo zitatolewa na madaktari bingwa wa macho kutoka Wizara ya Afya, ambao wamejipanga kufanya tathmini za kitaalamu kwa kila mgonjwa ili kubaini aina ya tatizo na kutoa matibabu yanayostahili.

Kwa mujibu wa msimamizi mkuu wa kambi hiyo Mussa Buluki, ambaye pia ni Katibu Mkuu wa taasisi ya The Islamic Foundation, lengo la kambi hiyo ni kuwafikia wananchi wenye uhitaji wa huduma za macho, hususan kutoka tabaka la watu masikini ambao mara nyingi hushindwa kumudu gharama za matibabu.

Kupitia mpango huo, baada ya kufanyiwa uchunguzi, wananchi waliougundulika kuwa na changamoto wanapewa dawa, miwani na wengine wenye mtoto wa jicho walifanyiwa upasuaji kurejesha uwezo wao wa kuona.

Kwa mujibu wa waandaaji, takribani wagonjwa 250 wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho bila malipo katika kipindi chote cha kambi hiyo. Hatua hiyo inatarajiwa kuwa msaada mkubwa kwa watu wengi ambao wamekuwa wakichelewesha matibabu kutokana na gharama za huduma hiyo.

Mtoto wa jicho ni miongoni mwa matatizo yanayoathiri uwezo wa kuona kwa watu wengi, hasa wazee, na endapo hautatibiwa kwa wakati unaweza kusababisha upofu wa kudumu.

Mbali na matibabu, wananchi waliofika katika kambi hiyo pia wamepata elimu kuhusu namna ya kutunza afya ya macho, dalili za awali za magonjwa ya macho na umuhimu wa kufanyiwa uchunguzi wa mara kwa mara.

Waandaaji wamewahimiza wananchi wa Morogoro na maeneo ya jirani kutumia fursa hiyo kwa kufika katika kituo hicho ili kupata huduma hizo bila malipo.

Kambi hiyo inaelezwa kuwa sehemu ya jitihada za wadau wa afya kushirikiana na Serikali katika kuongeza upatikanaji wa huduma za kitabibu kwa jamii, hasa katika maeneo ambayo baadhi ya wananchi hukumbana na changamoto za gharama na upatikanaji wa wataalamu bingwa.

Huduma hizo zinatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kuboresha maisha ya wananchi wengi kwa kuwasaidia kurejesha uwezo wa kuona na kuendelea na shughuli zao za kila siku kwa ufanisi zaidi.

ذُو الحِجَّة




# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar

0655 763 580

## Matibabu hayo yaliyoandaliwa na taasisi ya The Islamic Foundation kwa ufadhili wa Mercy Outreach Global
















ذُو الحِجَّة

**MAKALA ZA WAQF**

NA IDARA YA ELIMU – AWQAF TANZANIA

# Urithi usiokufa kupitia waqf wa fedha

Kila mwanadamu anatamani kuacha alama itakayodumu duniani hata baada ya kifo chake. Wengi wetu tunahangaika kujenga nyumba nzuri, kuweka akiba benki, au kurundika mali kwa ajili ya familia zetu. Hata hivyo, mara nyingi tunasahau kuandaa urithi wa kweli unaoweza kuendelea kutunufaisha hata tukiwa kaburini, urithi wa matendo mema yenye manufaa endelevu.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alituwekea msingi muhimu kupitia hadith iliyopokelewa na Abu Huraira (Allah amridhie), aliposema: "Mwanadamu anapokufa, matendo yake hukatika isipokuwa mambo matatu: sadaka yenye kuendelea (Sadaqatun Jariyah), elimu yenye manufaa, na mtoto mwema anayemuombea."

Katika njia hizi tatu, Waqf ni moja ya mifumo yenye nguvu zaidi kiuchumi na kiroho. Kupitia Waqf, mali binafsi hutengwa kwa ajili ya Allah Mtukufu ili manufaa yake yaendelee kuwafikia watu kwa muda mrefu bila kukatika.

## Asili ya waqf katika Uislamu

Historia ya Waqf inaanzia kwa Swahaba Umar bin Khattwab (Allah amridhie), alipokuwa na ardhi yenye thamani kubwa huko Khaybar. Alimshauri Mtume (Allah amshushie rehema na amani) kuhusu namna bora ya kuitumia, ndipo Mtume akamwambia aiweke asili ya ardhi hiyo salama na mapato yake yawasaidie maskini na wahitaji.

Umar (Allah amridhie) akaifanya ardhi hiyo kuwa Waqf wa kwanza katika Uislamu. Chanzo kikabaki salama, huku manufaa yake yakiendelea kuwafikia watu wengi.

Mfumo huu uliendelea kuimarika katika historia ya Kiislamu na kuwa nguzo muhimu ya elimu, afya, maji, na huduma za kijamii katika jamii nyingi za Kiislamu duniani.

## Nafasi ya Awqaf Tanzania

Hapa Tanzania, taasisi mpya ya Awqaf Tanzania inaendelea kuhamasisha na kusimamia Waqf kwa lengo la kukabiliana na changamoto mbalimbali za kijamii.

Kupitia taasisi hiyo pamoja na taasisi wanachama wake zaidi ya 50, mali kama nyumba, viwanja, mashamba, au hisa zinaweza kuwekwa wakfu kisheria ili mapato yake yaendelee kusaidia jamii.

Mapato hayo yanaweza kuelekezwa kusaidia wagonjwa waliokwama hospitalini, wanafunzi wanaokosa ada, miradi ya maji safi, pamoja na shughuli nyingine za maendeleo ya kijamii na Kiislamu.

## Cash Waqf: Fursa kwa kila Muislamu

Katika hatua mpya ya maendeleo, Awqaf Tanzania sasa inasimamia rasmi waqf wa fedha (cash waqf) wa Hay-at Ulamaa. Mfumo huu unafungua mlango kwa kila Muislamu kushiriki katika Waqf hata kama hana nyumba, shamba, au mali kubwa.

Kupitia Cash Waqf, mtu anaweza kuchangia kiasi chochote cha fedha taslimu. Fedha hizo hukusanywa pamoja na kuwekeza katika miradi halali inayozingatia misingi ya Sharia. Faida inayopatikana hutumika kusaidia shughuli za elimu, maendeleo ya jamii, kuwasaidia wanazuoni, pamoja na kuendesha miradi ya Kiislamu yenye manufaa kwa umma.

Hivyo, hata mchango mdogo unaweza kuwa sehemu ya urithi mkubwa unaoendelea kuleta manufaa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

## Hay-at Ulamaa na dhamira ya maendeleo

Unapozungumzia mustakabali wa Uislamu nchini Tanzania, ni vigumu kuiacha Hay-at Ulamaa. Taasisi hii imejijengea heshima kwa sababu ya misingi yake ya uadilifu, uwazi, na dhamira ya kuimarisha Waislamu kielimu, kiuchumi, na kijamii.

Katika kipindi ambacho taasisi nyingi zinakabiliwa na changamoto ya kupoteza uaminifu kwa jamii, Hay-at Ulamaa imeendelea kusimama kama taasisi inayosimamiwa na wanazuoni na walimu wenye historia ya kuitumikia dini kwa uaminifu. Ushirikiano wake na Awqaf Tanzania pia unaonesha dhamira ya kutumia mifumo ya kisasa ya utawala bora, ukaguzi wa hesabu, na uwazi wa matumizi ya rasilimali.

Mbali na kutoa elimu ya dini na fatwa, taasisi hii imeelekeza nguvu katika miradi ya muda mrefu inayolenga kujenga uwezo wa Waislamu kujitegemea kiuchumi na kielimu.

Mfumo wa uendeshaji wa Cash Waqf

Katika mfumo wa Cash Waqf, fedha zinazochangwa huhifadhiwa kama mtaji mkuu usioguswa. Kazi ya msimamizi wa Waqf (Mutawalli au Naadhwir) ni kuhakikisha fedha hizo zinawekezwa katika maeneo halali yenye tija na yanayozingatia misingi ya Kiislamu.

Uwekezaji unaweza kufanyika kupitia mifumo ya Kiislamu kama Sukuk (hati fungani), ushirikiano wa biashara (Musharaka), au uwekezaji wa Mudhwaraba. Lengo si kutumia mtaji wenyewe, bali kutumia faida inayopatikana kusaidia shughuli zilizokusudiwa.

Msimamizi wa Waqf pia anatakiwa kuhakikisha kuna uwazi wa hesabu, ukaguzi wa mara kwa mara, pamoja na ulinzi wa mtaji dhidi ya kupoteza thamani kutokana na mfumuko wa bei. Hii ndiyo siri ya kuhakikisha Waqf unaendelea kuwa na manufaa ya muda mrefu.



ذُو الحِجَّة

**HABARI** DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# DCEA YAONYA WANANCHI:

# "Nibebee kifurushi hiki" kunaweza kuwa ni mtego wa kukupeleka jela



**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imewaonya wananchi kuwa kubeba mzigo wa mtu asiyejulikana au kifurushi kisichofahamika kunaweza kuwa mtego unaotumiwa na wafanyabiashara wa dawa za kulevya kusafirisha bidhaa hizo haramu.**

Kitendo cha kumsaidia mtu kubeba kifurushi au mzigo wake wakati wa safari kinaweza kuonekana kuwa jambo la kawaida linaloonyesha utu, ukarimu na moyo wa kusaidiana. Hata hivyo, nyuma ya msaada huo wa kawaida kuna hatari kubwa inayoweza kumbadilishia mtu maisha, hasa pale mzigo huo unapobainika kuwa umebeba dawa za kulevya.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imewaonya wananchi kuwa tabia ya kukubali kubeba mizigo ya watu wasiowafahamu vizuri inaweza kuwa mwanzo wa matatizo makubwa ya kisheria, huku wahalifu wakitumia mwanya huo kuwahadaa wasafiri na wahudumu wa vyombo vya usafiri.

Tahadhari hiyo imetolewa baada ya kubainika kuwa mitandao ya usafirishaji wa dawa za kulevya imekuwa ikibadilisha mbinu na sasa kutumia abiria, makondakta, madereva na wananchi wa kawaida kusafirisha dawa hizo bila wao kujua kilichomo ndani ya vifurushi au mizigo wanayopewa.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, alisema wahalifu wamekuwa wakitumia hulka ya Watanzania kusaidiana na kuaminiana kama njia ya kufanikisha biashara yao haramu.

"Usikubali kubeba mzigo, kifurushi au bidhaa yoyote usiyoifahamu. Hakikisha unatambua unachobeba, kinatoka kwa nani na kinaelekea kwa nani. Kifurushi unachodhani ni cha kawaida kinaweza kubeba dawa za kulevya na kubadili maisha yako kwa matokeo hasi," alisema Lyimo.

Alisema baadhi ya wananchi wamejikuta wakikamatwa na kuhojiwa na vyombo vya dola baada ya kubeba mizigo waliyopewa na watu wasiowafahamu vizuri, wakiamini kuwa walikuwa wakitoa msaada wa kawaida tu.

Kwa mfano, msafiri anaweza kukutana na mtu katika kituo cha mabasi na kuombwa amfikishie ndugu yake kifurushi katika mkoa mwingine. Bila kuuliza maswali ya kina au kujua kilichomo ndani, anaweza kukubali kwa nia njema. Hata hivyo, endapo kifurushi hicho kitabainika kuwa na dawa za kulevya, msafiri huyo ndiye anayepaswa kueleza alikitoa wapi, alikipokea kutoka kwa nani na alikuwa akifahamu nini kuhusu yaliyomo ndani yake.

Mmoja wa wasafiri wanaosafiri mara kwa mara kati ya Dar es Salaam na Mwanza, ambaye hakutaka jina lake litajwe, alisema tahadhari hiyo ni muhimu kutokana na mazoea yaliyopo ya watu kusaidiana kubebeshana mizigo safarini.

"Watu wengi huomba msaada wa kubebewa mizigo bila kuulizwa maswali mengi. Baada ya kusikia matukio ya watu kukamatwa kwa sababu ya vifurushi wasivyovijua, sasa nimeamua kutokubali kubeba mzigo wowote ambao sijui chanzo chake," alisema.

Kwa mujibu wa DCEA, uchunguzi umeonyesha kuwa wafanyabiashara wa dawa za kulevya wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali kuficha dawa hizo kwenye mizigo inayoonekana kuwa ya kawaida ndani ya mabasi na vyombo vingine vya usafiri wa umma.

Takwimu za mamlaka hiyo zinaonyesha kuwa kuanzia Juni 2025 hadi Juni 2026, mabasi 15 yamekamatwa kutokana na kutumika katika usafirishaji wa dawa za kulevya, huku watumishi 41 wa mabasi hayo wakikamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Aidha, bodaboda 171 zimekamatwa katika kipindi hicho baada ya kubainika kutumika kusafirisha aina mbalimbali za dawa za kulevya.

Lyimo alisema baadhi ya madereva na makondakta wamejikuta wakiingia kwenye matatizo makubwa ya kisheria baada ya kukubali kubeba mizigo bila kujiridhisha kuhusu kilichomo ndani.

**Takwimu za mamlaka hiyo zinaonyesha kuwa kuanzia Juni 2025 hadi Juni 2026, mabasi 15 yamekamatwa kutokana na kutumika katika usafirishaji wa dawa za kulevya, huku watumishi 41 wa mabasi hayo wakikamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.**

NA MWANDISHI WETU

# ZANZIBAR YAFUNGUA UKURASA MPYA WA FEDHA:

# Soko la hisa na benki ya uwekezaji kuanza rasmi

Zanzibar imepanga kuanzisha soko lake la hisa pamoja na benki maalumu ya uwekezaji, hatua inayolenga kubadili mfumo wa upatikanaji wa mitaji kwa wafanyabiashara, taasisi za Serikali na wawekezaji katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

Mipango hiyo ni miongoni mwa vipaumbele vikuu vilivyotajwa na Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Dk. Juma Malik Akil, wakati akiwasilisha bajeti ya Sh8 trilioni kwa mwaka wa fedha 2026/27 katika Baraza la Wawakilishi jana.

Dk. Akil alisema Serikali itaongoza uanzishwaji wa Benki ya Uwekezaji ya Zanzibar (Zanzibar Investment Bank - ZIB) pamoja na Soko la Hisa la Zanzibar (Zanzibar Stock Market).

Hatua hiyo inaonyesha dhamira ya Zanzibar ya kuimarisha sekta ya fedha na kujenga njia mpya za kuvutia mitaji ya ndani na nje ya nchi, hasa katika maeneo muhimu kama utalii, miundombinu, uvuvi, uchumi wa bluu na viwanda.

Soko la hisa ni jukwaa ambalo kampuni na taasisi hutumia kupata fedha kwa kuuza hisa au dhamana, huku wawekezaji wakipata fursa ya kununua na kuuza mali hizo za kifedha.

Mbali na kusaidia biashara kupata fedha za muda mrefu, masoko ya hisa huongeza uwazi katika uendeshaji wa kampuni, kuimarisha utawala bora na kuwapa wananchi nafasi ya kushiriki katika ukuaji wa uchumi kupitia uwekezaji.

Kwa Zanzibar, soko maalumu la hisa linaweza kutoa mbadala kwa wafanyabiashara wanaotegemea mikopo ya benki pekee, kwa kuwa wataweza kupata mitaji moja kwa moja kutoka kwa wawekezaji.

Aidha, wananchi wa Zanzibar wataweza kupata fursa ya kuwekeza katika kampuni za ndani na kunufaika na ukuaji wa uchumi wa visiwa hivyo.

Benki ya uwekezaji inayopangwa kuanzishwa inatarajiwa kuimarisha uwepo wa soko hilo kwa kusaidia ufadhili wa miradi mikubwa na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Kwa kawaida, benki za uwekezaji husaidia kupanga miamala mikubwa ya kifedha, kushauri kampuni kuhusu namna ya kupata mitaji na kusaidia biashara kupanua shughuli zao.

Hatua hiyo itaifanya Zanzibar kuingia katika kundi la maeneo ya Afrika Mashariki yenye mifumo ya masoko ya mitaji, yakiongozwa na nchi kama Kenya, Tanzania, Uganda na Rwanda.

Kwa sasa, ukanda huo una masoko ya hisa kama Soko la Hisa la Nairobi, Soko la Hisa la Dar es Salaam, Soko la Hisa la Uganda na Soko la Hisa la Rwanda, ambayo yanawezesha biashara ya hisa, dhamana na bidhaa nyingine za kifedha.

Soko la Hisa la Dar es Salaam lilianzishwa mwaka 1996 na kuanza shughuli za biashara mwaka 1998. Linatoa huduma za biashara ya hisa, dhamana na mifuko ya uwekezaji wa majengo (REITs), chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA).

"Katika kipindi hiki, wizara itaanzisha Soko la Hisa la Zanzibar na benki ya uwekezaji," alisema Dk. Akil akiwaeleza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.





Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Dk. Juma Malik Akil

■ Yajipanga kuingia katika kundi la nchi zenye masoko ya hisa kama Tanzania (Soko la Hisa la Dar es Salaam), Kenya (Soko la Hisa la Nairobi), Uganda (Soko la Hisa la Uganda) na Rwanda (Soko la Hisa la Rwanda).

ذُو الحِجّة

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWAJUMA SALUM, BAGAMOYO



# Wazazi wahimizwa kuwapa watoto majina yenye kheri

Wazazi wamehimizwa kuwapa watoto wao majina yenye maana nzuri na kheri, kwani majina hayo yanaweza kuwa dua njema na mchango muhimu katika maisha yao.

Rai hiyo imetolewa na Sheikh Sharqawi Ramadhani Wawa wakati wa kongamano la kidini lililofanyika katika Madrasat Madyani, wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.

Sheikh Wawa alisema baadhi ya wazazi huwapa watoto majina bila kufahamu maana zake, jambo ambalo linaweza kuwa na athari kwa watoto hao wanapokuja kugundua maana halisi ya majina yao.

"Ni muhimu wazazi kuhakikisha wanawapa watoto majina yenye maana nzuri na yenye kheri. Si vyema kumpa mtoto jina ambalo hulijui maana yake," alisema.

Aliongeza kuwa baadhi ya wazazi wamekuwa wakichagua majina kutoka katika tamthilia au filamu mbalimbali bila kuzingatia maana zake, hali inayowafanya baadhi ya watoto kukataa majina yao wanapokuwa watu wazima baada ya kufahamu maana halisi ya majina hayo.

Aidha, aliwataka wazazi kujiepusha na tabia ya kuwatukana watoto au kuwatamkia maneno mabaya wanapokosea, akisema maneno hayo yanaweza kuwa na athari kwa malezi yao. Badala yake, aliwashauri wazazi kutumia busara, hekima na maneno yenye mawaidha na kheri wakati wa kuwaadabisha watoto ili kuwasaidia kurekebisha makosa yao.

Katika hatua nyingine, Sheikh Wawa aliwahimiza wazazi kuwapeleka watoto madrasa ili wapate elimu ya dini na maadili mema yatakayowasaidia katika maisha ya dunia na Akhera. Alisema malezi bora yanahitaji wazazi kuwa mstari wa mbele kuwaongoza watoto katika njia sahihi kwa kuwajengea msingi wa kumcha Mwenyezi Mungu tangu wakiwa wadogo.

# Wananchi wapongeza ujenzi wa zahanati Bagamoyo

Wananchi wa Kitongoji cha Mtakuja, Kata ya Fukayosi wilayani Bagamoyo, wameishukuru Serikali kwa ujenzi wa zahanati iliyowapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya.

Wakizungumza wakati wa uzinduzi wa zahanati hiyo uliofanywa na Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, Subira Mgalu, wananchi walisema awali walilazimika kutumia muda na gharama kubwa za usafiri kufuata matibabu katika maeneo ya mbali. Mganga Mkuu wa zahanati hiyo, Michael Kazamba, alisema zaidi ya wagonjwa 100 wamehudumiwa ndani ya mwezi mmoja tangu kituo hicho kifunguliwe.

Katika hafla hiyo, Mgalu alisema ataendelea kutafuta ufumbuzi wa changamoto za miundombinu ya barabara katika kata hiyo, huku Diwani wa Fukayosi, Mrisho Some, akipongeza juhudi za Serikali za kupeleka huduma za umeme na maendeleo mengine kwa wananchi.

UKHT FATIMA SS

# Uganda yahimizwa kuharakisha utoaji ithibati Halal




***KAMPALA, Uganda*** – Wataalamu wameitaka Uganda kuharakisha utoaji wa vyeti vya Halal katika sekta za utalii, hoteli na huduma za chakula kabla ya mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027, wakisema hatua hiyo inaweza kuleta manufaa ya kiuchumi ya muda mrefu hata baada ya mashindano hayo kumalizika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Halal Assurance Institute Uganda, Ali Kalema, amesema AFCON 2027 ni fursa muhimu kwa Uganda kujitangaza kama kitovu cha utalii na uwekezaji rafiki kwa Waislamu barani Afrika.

"AFCON 2027 si tukio la michezo pekee, bali ni lango la Uganda kuingia katika uchumi mkubwa wa Halal unaokua kwa kasi duniani," alisema Kalema.

Alieleza kuwa uchumi wa Halal, unaojumuisha chakula, utalii, fedha, dawa na usafirishaji, unahudumia zaidi ya Waislamu bilioni mbili duniani na ni miongoni mwa sekta zinazokua kwa kasi zaidi.

Kwa mujibu wa Kalema, hoteli, migahawa na vituo vya utalii vitakavyopata vyeti vya Halal vitaongeza imani kwa wageni wa kimataifa na kuvutia watalii pamoja na wawekezaji kutoka Mashariki ya Kati, Afrika Kaskazini na Asia. Aliongeza kuwa mfumo imara wa Halal unaweza pia kuchochea ukuaji wa sekta za kilimo, mifugo, dawa, vipodozi na fedha za Kiislamu, huku ukifungua maelfu ya nafasi za ajira na kuongeza mauzo ya bidhaa za Uganda katika masoko ya kimataifa.

# Waislamu Uganda: Mashujaa wetu nao watambuliwe kitaifa

***KAMPALA, Uganda*** – Viongozi wa Kiislamu kutoka maeneo ya Teso na Karamoja wameiomba serikali ya Uganda kutambua na kuheshimu zaidi ya mashujaa 70 wa Kiislamu waliouawa kati ya mwaka 1875 na 1876 wakati wa utawala wa Kabaka Muteesa I wa Buganda.

Wito huo umetolewa wakati Uganda ilipoadhimisha Siku ya Mashujaa wa Kidini (Martyrs Day), Juni 3 kila mwaka, ambayo kwa kawaida huwakumbuka Wakristo 45 waliouawa kwa sababu ya imani yao mwaka 1886.

Sheikh Abubakar Umar Obilan, Msaidizi wa Mufti wa Mkoa wa Kaskazini Mashariki wa Baraza Kuu la Waislamu Uganda, amesema mashujaa hao wa Kiislamu walikuwa miongoni mwa Waganda wa kwanza kujitoa mhanga kwa ajili ya imani yao na wanastahili kutambuliwa kama sehemu ya urithi wa taifa.

Kwa mujibu wa viongozi hao, Waislamu hao waliuawa baada ya kukataa kuacha mafundisho ya Uislamu na kutii baadhi ya amri zilizokuwa zinakinzana na imani yao. Wanasema historia yao haijaandikwa wala kufahamika kwa kiwango sawa na ile ya mashujaa wa Kikristo.

Viongozi hao wameitaka serikali kushirikiana na wanahistoria na watafiti ili kutambua maeneo muhimu ya kihistoria na kuhakikisha mchango wa mashujaa wa dini zote unatambuliwa katika simulizi rasmi la taifa.




# Misikiti 15 yafungwa India

Serikali ya jimbo la Arunachal Pradesh imefunga misikiti 15 kwa kukosa vibali katika mji mkuu wa Itanagar na kuibua malalamiko makubwa ya kubaguliwa kutoka kwa Waislamu, inaripoti tovuti ya Muslim Network.

Waislamu wanasema hatua hiyo imelenga taasisi za Kiislamu pekee huku ikiacha maeneo mengine ya ibada bila uchunguzi sawa. Viongozi wa Kiislamu wameitaka serikali kufungua tena misikiti hiyo na kuhakikisha sheria zinatumika kwa usawa kwa dini zote.

Hata hivyo, Kamati ya Ustawi wa Misikiti ya Arunachal imesema kuwa ikiwa suala ni nyaraka na vibali, basi makanisa, mahekalu na maeneo mengine ya ibada yanapaswa pia kufanyiwa uhakiki kwa viwango sawa.

Mvutano huo umeibuka baada ya shinikizo kutoka kwa makundi ya vijana wa asili waliodai kuwepo kwa miundombinu isiyoidhinishwa.

Baadhi ya Waislamu wamedai kuwa kwa miezi kadhaa taasisi za Kiislamu zimekuwa zikikabiliwa na mazingira magumu, huku vituo kadhaa vya elimu ya dini vikifungwa kutokana na presha za kijamii na kisiasa.

India ina Waislamu zaidi ya milioni 200 (asilimia 14 ya wakazi wote) na kuifanya kuwa moja ya jamii kubwa zaidi za Kiislamu duniani.

# Misikiti Ireland yasimamisha ibada kuhofia kushambuliwa

BELFAST, Ireland Kaskazini – Waislamu nchini Ireland Kaskazini wanaendelea kuishi kwa hofu kufuatia siku kadhaa za ghasia na mashambulizi yaliyolenga wahamiaji na watu wa makundi ya wachache baada ya shambulio la kisu lililohusishwa na mwomba hifadhi kutoka Sudan.

Vurugu hizo, ambazo zimesababisha kuchomwa moto kwa nyumba, magari na mabasi katika maeneo mbalimbali ya Belfast na miji ya jirani, zimelazimu baadhi ya misikiti kusitisha shughuli za ibada huku wazazi wakiwazuia watoto wao kwenda shule kutokana na wasiwasi wa usalama huku wengine wakitafuta makazi ya muda.

Taarifa zinasema mitandao ya kijamii imechangia pakubwa kuchochea chuki dhidi ya wahamiaji na Waislamu ambapo video za tukio hilo zilienea kwa kasi mtandaoni, hususan Whatsapp na X, huku wanaharakati wa mrengo mkali wa kulia wakitumia tukio hilo kuhamasisha maandamano na kampeni za kupinga uhamiaji yaliyogeuka kuwa ghasia na vurugu.

Wachambuzi wa masuala ya kijamii wanaonya kuwa taarifa za upotoshaji na simulizi zinazowahusisha wahamiaji na uhalifu zimekuwa zikienezwa kwa muda mrefu, hali iliyochangia kuongezeka kwa hasira dhidi ya makundi ya wachache.

Takwimu zinaonesha kuwa Waislamu ni takribani 15,000 pekee kati ya wakazi zaidi ya milioni mbili wa Northern Ireland, chini ya asilimia moja ya idadi ya watu wote.

"Tunaunda chini ya asilimia moja ya wakazi wa Ireland Kaskazini, lakini kwa muda mrefu tumekuwa tukichorwa kama tishio kwa jamii," alisema mmoja wa viongozi wa Kiislamu ambaye hakutaka kutajwa jina lake kwa sababu za kiusalama.

**MAKALA MAALUM**

SEHEMU YA **1**

Na Said Rajab
0783 650 803



# VITA MASHARIKI YA KATI:
# Pakistan ni msuluhishi halisi au kibaraka wa Marekani?

Nyuma ya lugha ya upatanishi katika vita ya Marekani na Israel dhidi ya Iran, kuna mtindo unaojulikana wa utegemezi ambapo Pakistan inafanya kazi ndani ya mfumo ambao haina uwezo wa kuudhibiti.

Ndugu msomaji, fuatana nami katika makala haya yenye mafunzo makubwa.

# Pakistan ni msuluhishi halisi au kibaraka wa Marekani?

Nyuma ya lugha ya upatanishi katika vita ya Marekani na Israel dhidi ya Iran, kuna mtindo unaojulikana wa utegemezi ambapo Pakistan inafanya kazi ndani ya mfumo ambao haina uwezo wa kuudhibiti.

Ndugu msomaji, fuatana nami katika makala haya yenye mafunzo makubwa.

## Usuli

Tangu mwishoni mwa mwezi Februari mwaka huu, vita ya Marekani na Israel dhidi ya Iran imepandisha bei ya mafuta na kuathiri masoko ya bidhaa hiyo duniani kote.

Mapema mwezi Aprili 2026, Pakistan ilijitokeza kama mpatanishi katika mazungumzo ya kusitisha mapigano, ikijiweka kama daraja kati ya nchi hizo zinazopigana, licha ya kuwa na uhuru mdogo wa kuliendea jambo hilo.

Kati ya mwezi Machi na Aprili 2026, mashambulizi ya Mazayuni dhidi ya Lebanon yaliua watu 2,294 na kuwafanya wengine zaidi ya milioni moja kuyahama makazi yao, huku vita dhidi ya Iran vikisababisha vifo vya maelfu ya raia.

Aprili 8, 2026, usitishaji wa muda wa mapigano ulitangazwa kufuatia wiki kadhaa za mazungumzo ya kidiplomasia yaliyowahusisha wapatanishi wa kikanda.

Taarifa zilizokuja baadaye zilieleza kuwa Iran iliufunga tena Mlango–Bahari wa Hormuz baada ya kuufungua kwa muda mfupi kufuatia kauli ya Marekani kwamba ingeendeleza vikwazo vyake dhidi ya bandari za Iran.

Jambo la ajabu ni kwamba Pakistan haiwezi hata kutatua matatizo yake yenyewe, lakini inajishughulisha na vita ya Marekani na Iran. Tuwe wakweli. Pakistan haiwezi hata kutuliza migogoro yake ya ndani, lakini sasa inataka kutuliza vita kati ya Marekani na Iran.

Hii imekaaje? Pakistan imekuwa ikigonga vichwa vya habari duniani kote kama mpatanishi kati ya Iran na Marekani. Hebu tuangalie suala hili kwa umakini zaidi.

Waziri Mkuu wa Pakistan, Shehbaz Sharif, alimpendekeza mara mbili Rais wa Marekani, Donald Trump kwa ajili ya kupewa Tuzo ya Amani ya Nobel ya mwaka 2025, licha ya kuwepo kwa mauaji ya halaiki ya Gaza ambayo Trump aliyaunga mkono.

Wakati wa kusainiwa kwa kile kilichoitwa "Mkataba wa Amani wa Gaza" Oktoba 13 mwaka jana, Shehbaz alimsifu sana Donald Trump katika moja ya nyakati za kufedhehesha zaidi katika uhusiano wa kimataifa.

Viongozi mbalimbali walioiongoza Pakistan wamekuwa hawana utashi, na pia hawana uwezo wa kutatua mateso ya watu wa Kashmir kwa miongo kadhaa. Pakistan haiwezi kushughulikia mvutano na jirani yake Muislamu, Afghanistan, bila kulipua mabomu na kuua maelfu ya watu.

Aidha, imetumia miongo kadhaa kupigana vita ya Marekani inayojulikana kama Vita dhidi ya Ugaidi (War on Terror) kwa gharama ya makumi ya maelfu ya watu wake. Lakini sasa, ghafla imegeuka kuwa "mleta amani".

Pakistan inadai ilisaidia kuratibu usitishaji wa mapigano baada ya siku 40 za kuongezeka kwa mapigano kati ya Marekani na Israel dhidi ya Iran. Je, unaamini hilo, au kuna jambo lingine linaloendelea hapa?

## Mpatanishi au kibaraka wa Marekani?

Hata usitishaji wa mapigano unaoonekana sasa, ambao tunaambiwa Pakistan imeshiriki katika upatanishi, unazua swali la msingi: je, unamaanisha nini hasa?

Je, ni ushawishi unaojitegemea, nguvu isiyoegemea upande wowote, au uwezo wa kushinikiza pande zote mbili ili kufinyanga matokeo yanayotarajiwa.

Tunapowaangalia wapatanishi halisi katika siasa za kimataifa, tunaona kuwa wana ushawishi juu ya pande zote mbili zinazokinzana. Pakistan haina chochote kati ya hivyo. Inafanya kazi kwa utegemezi, si kwa ushawishi.

*Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah*






MAKALA MAALUM

Na Abeid Othman
0754 990 083

# Misikiti irudi kuwa vituo vya kuutumikia umma

**Katika historia ya Uislamu, msikiti haukuwa tu mahali pa kuswali. Ulikuwa moyo wa jamii, kitovu cha mshikamano, darasa la elimu, mahakama ya haki, na kimbilio la wanyonge.**
**Leo hii, katika maeneo mengi, misikiti imebaki kuwa sehemu za kutekeleza ibada ya swala pekee, huku jukumu lake la kijamii likizidi kufifia.**

Ni wakati wa kujiuliza kwa dhati: je, misikiti yetu inawajua waumini wake? Je, inatambua wajane, yatima, walemavu na wahitaji wanaoishi mita chache kutoka milango yake?

Katika hali ya sasa, misikiti mingi haijui hata idadi ya Waislamu wanaoishi katika eneo lake. Hakuna takwimu za familia zenye uhitaji maalum, hakuna orodha ya wajane wanaohitaji msaada wa kimaisha, hakuna utambuzi wa vijana waliokata tamaa au walioko kwenye hatari ya kujiingiza katika maovu.

Msikiti unafunguliwa wakati wa swala, waumini wanaingia, wanaswali na kuondoka. Uhusiano unabaki kuwa wa haraka na wa juu juu. Hakuna mfumo wa kufuatilia hali za waumini, wala jukwaa la kuzijadili changamoto zao kwa pamoja.

Wajane wengi katika jamii zetu wanabeba mizigo mizito kimya kimya. Yatima wanakua bila uangalizi wa karibu wa kijamii. Walemavu wanajikuta wamesahaulika, hata miundombinu ya misikiti mingine haiwazingatii kwa kuwajengea mazingira rafiki. Lakini misikiti ipo katikati ya mitaa yao.

Hili ni pengo kubwa kati ya dhamira ya Uislamu na uhalisia wa leo. Dini inasisitiza kuwajali wahitaji, lakini taasisi kuu ya dini katika jamii yaani msikiti, imejikita zaidi katika ibada kuliko huduma ya kijamii.

## Msikiti wa Mtume

Tukirudi katika historia, tunaona picha tofauti kabisa kupitia Msikiti wa Mtume ulioko Madina, Al-Masjid an-Nabawi. Msikiti huu haukuwa tu sehemu ya kuswali, bali ulikuwa makao makuu ya dola ya Kiislamu.

Ndani yake, Mtume Muhammad (Rehema na amani zimshukie) aliongoza mikutano ya kijamii, alipokea wajumbe kutoka makabila mbalimbali, alitoa hukumu za kisheria, na kupanga mikakati ya kulinda na kuendeleza jamii ya Waislamu. Masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yalijadiliwa hapo hapo.

Katika msikiti huo, kulikuwa na kundi la watu waliokuwa wakijulikana kama Ahlus-Suffah yaani maswahaba maskini waliokuwa hawana makazi wala mali. Waliishi katika eneo la msikiti, wakipewa malezi, chakula na elimu.

Hii ilikuwa ishara tosha kwamba msikiti haukuwa na mipaka ya ibada pekee, bali ulikuwa hifadhi ya kijamii. Hakuna aliyekuwa akilala njaa bila jamii kujua. Hakuna mjane au yatima aliyekuwa nje ya uangalizi wa umma.

Msikiti wa Mtume pia ulikuwa chuo. Maswahaba walijifunza Qur'ani, hadithi na maarifa ya maisha humo humo. Vijana walipata mafunzo ya maadili na uwajibikaji. Wanawake walikuwa na nafasi ya kuuliza maswali na kushiriki katika masuala ya kijamii. Kwa maneno mengine, msikiti ulikuwa shule, ofisi ya ustawi wa jamii, na kituo cha maamuzi kwa wakati mmoja.

Leo hii, tuna misikiti mizuri yenye majengo ya kuvutia na minara mirefu, lakini je, ndani yake kuna mifumo ya kusaidia jamii? Je, kuna kamati maalum za kutembelea wagonjwa, kufuatilia familia zenye migogoro, au kusaidia vijana kupata ajira?



Je, kuna hazina za kusaidia ada za yatima au mitaji midogo kwa wajane? Mara nyingi, michango hukusanywa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati, lakini michango ya kuendeleza maisha ya watu inakuwa midogo au isiyo na uratibu wa kudumu.

## Tufanye haya

Ili misikiti irudi kuwa vituo vya kuutumikia umma, kunahitajika mabadiliko ya kimtazamo na kiutendaji. Kwanza, kila msikiti unapaswa kuwa na takwimu za waumini wake.

Misikiti ijue ni familia ngapi zipo, changamoto zao ni zipi, na ni rasilimali gani zinahitajika. Pili, kuwe na kamati za ustawi wa jamii zitakazoshughulikia moja kwa moja masuala ya wajane, yatima, walemavu na wahitaji wengine.

Tatu, misikiti iwe na programu za elimu ya maisha kwa vijana, mafunzo ya ndoa, na hata semina za ujasiriamali.

Viongozi wa misikiti wanapaswa kuona jukumu lao likizidi lile la kutoa khutba za Ijumaa pekee. Wanapaswa kuwa wasimamizi wa ustawi wa kijamii, washauri wa familia, na waunganishi wa rasilimali ndani ya jamii.

Ushirikiano na taasisi nyingine za kijamii unaweza kuimarisha huduma hizi. Msikiti unaweza kuwa daraja kati ya matajiri na maskini, kati ya wenye elimu na wasio na elimu, kati ya wenye nguvu na wanyonge.

Zaidi ya yote, ni lazima kurejesha roho ya uwajibikaji wa kijamii miongoni mwa waumini wenyewe. Msikiti si jengo tu; ni watu.

Ikiwa kila muumini atahisi kuwa ana jukumu la kumjua jirani yake, kumtembelea mgonjwa, au kumsaidia yatima, basi msikiti utarejea kuwa kitovu cha mshikamano.

Historia inatufundisha kwamba ustaarabu wa Kiislamu ulijengwa juu ya misingi ya mshikamano na huduma kwa jamii, si ibada ya peke yake.

Tukirejesha misikiti katika nafasi yake halisi kama vituo vya kuutumikia umma, tutajenga jamii imara, yenye huruma, na inayojali kila mmoja. Huo ndio urithi wa Msikiti wa Mtume, na huo ndio wajibu wetu leo.

UKHTI FATIMA SS




# Fitch: Ukwasi wa Sukuk waanza kuimarika baada ya vita vya Iran

Wakala wa kimataifa wa ukadiriaji wa mikopo, Fitch Ratings, umesema ukwasi katika soko la sukuk duniani umeanza kuimarika taratibu baada ya kuyumba kufuatia vita vya Iran, ingawa bado haujafikia viwango vilivyokuwapo kabla ya mzozo huo.

Katika ripoti yake ya karibuni ikinukuliwa na tovuti la Arab News, Fitch imeeleza kuwa sukuk nyingi zilizokadiriwa na taasisi hiyo zimeonesha kuongezeka kwa ukwasi, ishara ya kurejea kwa utulivu katika soko la hati fungani zinazozingatia misingi ya Sharia. Hata hivyo, Fitch imeonya kuwa hali ya ukwasi itaendelea kuwa chini ya viwango vya kabla ya vita kwa muda wote ambao mgogoro huo utaendelea.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, sukuk zenye daraja la juu la uwekezaji (investment-grade) zimeendelea kuwa na ukwasi mkubwa zaidi, zikifikia wastani wa alama 66 mwezi Juni kutoka alama 64 mwezi Machi, ingawa bado ziko chini ya alama 72 zilizorekodiwa Januari.

Fitch imesema sukuk za serikali zimechangia kwa kiwango kikubwa kuimarika kwa ukwasi huo, huku wawekezaji wakionekana kuwa na imani zaidi katika hati fungani zinazoungwa mkono na serikali na taasisi zenye uwezo mkubwa wa kifedha.

Ripoti hiyo imebainisha kuwa Malaysia, ambayo inachangia takribani asilimia 60 ya soko la sukuk duniani kwa ujazo, imeendelea kuwa miongoni mwa masoko yenye ukwasi mkubwa zaidi. Sukuk za Saudi Arabia, Qatar, Kuwait na Indonesia pia zimeendelea kufanya vizuri.



UKHTI FATIMA SS




# Indonesia yatoa somo ujenzi wa mfumo wa uchumi wa Kiislamu

Wakati nchi nyingi zenye Waislamu wengi zikiendelea kutafuta njia za kukuza uchumi wa Kiislamu, Indonesia inaibuka kama mfano wa jinsi sekta hiyo inaweza kutumika kama chombo cha maendeleo ya kiuchumi, ujumuishi wa kifedha na kushindana kimataifa.

Indonesia imechukua mkakati mpana kujenga mfumo kamili wa uchumi wa Kiislamu unaounganisha uzalishaji, biashara, uwekezaji na fedha.

Kwa mujibu wa uchambuzi uliochapishwa na The Diplomatic Insight, matumizi ya Waislamu duniani katika sekta za Halal yalifikia dola trilioni 2.4 mwaka 2023 na yanatarajiwa kuvuka dola trilioni 3.4 ifikapo mwaka 2028. Wakati huo huo, thamani ya mali katika sekta ya fedha za Kiislamu imefikia karibu dola trilioni 4.9, jambo linaloifanya sekta hiyo kuwa miongoni mwa maeneo yanayokua kwa kasi katika uchumi wa dunia.

Katika mazingira hayo, Indonesia, taifa lenye Waislamu wengi kuliko nchi nyingine yoyote ni ya tatu bora katika Viashiria vya Uchumi wa Kiislamu vya Kidunia kutokana na mafanikio yake katika sekta za mavazi ya staha, utalii rafiki kwa Waislamu na bidhaa za Halal.

Kinachofanya Indonesia kuwa mfano wa kuigwa si ukubwa wa soko lake pekee, bali namna ilivyobadili uchumi wa Kiislamu kutoka kuwa suala la matumizi ya bidhaa za Halal na kuligeuza kuwa mkakati wa maendeleo ya taifa.

Tofauti na baadhi ya nchi ambazo zimejikita katika benki za Kiislamu pekee, Indonesia imeunganisha sekta mbalimbali ikiwemo chakula cha Halal, utalii rafiki kwa Waislamu, mavazi ya staha, fedha za Kiislamu, wakfu na biashara ndogo ndogo. Mfumo huu umeifanya sekta hiyo kukua kwa kasi kuliko uchumi wa taifa kwa ujumla.

Wafanyabiashara wadogo na wa kati huwezeshwa kupata mitaji, vyeti vya Halal na masoko ya bidhaa zao kwa wakati mmoja. Hivyo, fedha za Kiislamu zinatumika kuchochea uzalishaji na biashara badala ya kubaki katika shughuli za kifedha pekee.

Sehemu muhimu ya mkakati huo ni Festival Ekonomi Syariah (FESYAR), jukwaa linalowakutanisha watunga sera, benki, wafanyabiashara, vyuo, taasisi za waqf na vijana wajasiriamali. Kupitia jukwaa hilo, Indonesia hujenga mazingira yanayounganisha uzalishaji, upatikanaji wa mitaji, uthibitishaji wa Halal na upatikanaji wa masoko.

Benki Kuu ya Indonesia nayo imepewa jukumu pana zaidi ya kudhibiti mfumuko wa bei. Kupitia sera zake, imekuwa ikikuza masoko ya fedha za Kiislamu, kuhimiza matumizi ya teknolojia za kidijitali na kusaidia ujumuishaji wa sekta za Halal katika mfumo wa kifedha wa taifa.

Hata hivyo, Indonesia bado inakabiliwa na changamoto za kuoanisha viwango vya kimataifa vya vyeti vya Halal na kuongeza ushawishi wake katika kutunga kanuni za kimataifa za uchumi wa Kiislamu. Pamoja na changamoto hizo, hatua iliyofikiwa inaifanya kuwa miongoni mwa mifano bora duniani.

Katika kipindi ambacho dunia inatafuta mifumo ya uchumi inayojali maadili, ujumuishi na maendeleo endelevu, Indonesia imeonesha kuwa uchumi wa Kiislamu unaweza kuwa zaidi ya huduma za benki. Unaweza kuwa mkakati wa kitaifa wa maendeleo unaounganisha ukuaji wa uchumi, haki ya kijamii na ustawi wa wananchi.

Uzoefu wa Indonesia unaonesha kuwa mafanikio ya uchumi wa Kiislamu hayajengwi kwa hatua za haraka, bali kwa mkakati wa muda mrefu unaounganisha taasisi, sera na wadau mbalimbali. Ndiyo sababu leo Indonesia haionekani tu kama soko kubwa la bidhaa za Halal, bali kama maabara ya sera za uchumi wa Kiislamu ambayo mataifa mengine yanaanza kujifunza.

Kwa nchi za Afrika, hususan Tanzania, somo kuu kutoka Indonesia ni kwamba maendeleo

# Jukwaa la kimataifa fedha za Kiislamu kujadili ukuaji endelevu Azerbaijan

**BAKU, Azerbaijan – Wadau sekta ya fedha kutoka duniani kote watakutana Juni 17 mjini Baku katika Jukwaa la 20 la Kimataifa la Fedha za Kiislamu linaloandaliwa na Islamic Development Bank Institute (IsDBI).**

**Mkutano huo utabeba kaulimbiu isemayo "Kufikia Ustawi Endelevu Kupitia Fedha za Kiislamu."**

**Waandaaji wanasema jukwaa hilo litajadili namna fedha za Kiislamu zinavyoweza kusaidia nchi kukabiliana na vikwazo vya maendeleo, kuimarisha ukuaji jumuishi wa uchumi na kuongeza ustahimilivu dhidi ya misukosuko ya kiuchumi duniani.**

**Miongoni mwa mada kuu zitakazojadiliwa ni matumizi ya fedha za kijamii za Kiislamu, hususan mifumo ya waqf, katika kusaidia usalama wa chakula na nishati, pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi kati ya nchi wanachama wa Benki ya Maendeleo ya Kiislamu. Jukwaa hilo pia litashuhudia kutangazwa kwa washindi wa shindano la matumizi ya Akili Mnemba (AI) katika sekta ya fedha za Kiislamu, huku Mtendaji Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Biashara na Fedha la IsDB (ITFC), Adeeb Yousuf Al Aama akitajwa mmoja wa watoa mada.**

**Waandaaji wanatarajia mkutano huo kutoa mapendekezo yatakayochochea ubunifu, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kuharakisha ukuaji wa sekta ya fedha za Kiislamu duniani.**



# Hatua sita za kuanza uwekezaji kwa mafanikio

**Watu wengi wangependa kuwekeza lakini hawajui waanzie wapi. Wengine huamini kuwa uwekezaji ni shughuli ya matajiri pekee, huku wengine wakisubiri hadi wapate mtaji mkubwa kabla ya kuanza. Ukweli ni kwamba safari ya uwekezaji huanza kwa maandalizi sahihi kuliko ukubwa wa fedha ulizonazo. Wataalamu wa fedha wanaeleza kuwa mafanikio katika uwekezaji hayategemei bahati, bali hutokana na nidhamu, maarifa na mipango ya muda mrefu.**

## Jenga msingi imara wa kifedha

Kabla ya kuwekeza, ni muhimu kwanza kuhakikisha hali yako ya kifedha iko katika msingi mzuri.

Moja ya mambo muhimu ni kuwa na akiba ya dharura inayoweza kugharamia matumizi ya miezi mitatu hadi sita iwapo utapoteza kipato au kukumbwa na changamoto zisizotarajiwa.

Pia ni busara kupunguza au kuondoa madeni yanayokuletea mzigo mkubwa wa kifedha. Muislamu anapaswa kuwa mwangalifu na madeni yenye riba na kutafuta njia mbadala zinazokubalika kisheria na kidini.

Aidha, ni muhimu kuwa na bajeti inayokusaidia kujua mapato na matumizi yako kabla ya kufikiria uwekezaji.

## Tambua lengo la uwekezaji

Kila uwekezaji unapaswa kuwa na kusudi maalumu.

Je, unawekeza kwa ajili ya elimu ya watoto? Unajiandaa kwa maisha ya uzeeni? Unakusudia kununua nyumba? Au unataka kuongeza thamani ya mali zako kwa muda mrefu?

Majibu ya maswali haya yatasaidia kuchagua aina ya uwekezaji inayokufaa. Mtu anayejiandaa kwa gharama za miaka 20 ijayo anaweza kuchukua mikakati tofauti na anayehitaji fedha ndani ya miaka miwili au mitatu.

## Jifunze misingi ya uwekezaji

Kabla ya kuweka fedha zako mahali popote, ni muhimu kuelewa kanuni za msingi za uwekezaji.

Miongoni mwa mambo muhimu ni kuelewa uhusiano kati ya faida na hatari. Kwa kawaida, uwekezaji wenye matarajio ya faida kubwa huwa na kiwango kikubwa zaidi cha hatari.

Ni muhimu pia kuelewa dhana ya kugawanya uwekezaji katika maeneo tofauti badala ya kuweka fedha zote sehemu moja. Mbinu hii husaidia kupunguza madhara endapo sekta moja itakumbwa na changamoto.

Kwa Muislamu, hatua hii pia inajumuisha kuhakikisha uwekezaji unaochaguliwa unaendana na misingi ya Sharia na hauhusiani na shughuli zilizokatazwa kama vile riba, kamari au biashara za bidhaa haramu.

## Chagua eneo la kuwekeza

Baada ya kujifunza misingi, hatua inayofuata ni kuchagua sehemu ya kuwekeza.

Baadhi ya watu huwekeza katika biashara zao wenyewe, wengine huwekeza katika hisa za kampuni, mali isiyohamishika kama viwanja na nyumba, au bidhaa za uwekezaji zinazofuata misingi ya fedha za Kiislamu.

Kwa wanaoanza, wataalamu wengi hushauri kuanza na uwekezaji unaoueleweka vizuri badala ya kufuata tu mitindo au ahadi za kupata utajiri wa haraka.

Kumbuka kwamba uwekezaji mzuri ni ule unaoeleweka, unaolindwa na sheria na unaozalisha thamani halisi katika uchumi.

## Kuwa na nidhamu na uthabiti

Moja ya siri kubwa za mafanikio katika uwekezaji ni uthabiti.

Badala ya kusubiri uwe na fedha nyingi sana, unaweza kuanza kwa kiasi kidogo na kuongeza hatua kwa hatua kadiri kipato kinavyokua. Watu wengi waliofanikiwa kifedha walijenga mali zao kwa kuwekeza kiasi kidogo mara kwa mara kwa muda mrefu.

Changamoto nyingine ni kuruhusu hisia kutawala maamuzi. Mara nyingi watu huingiwa na hofu wakati soko linaporudi nyuma au tamaa wakati bei zinapopanda sana. Nidhamu huwasaidia wawekezaji kufanya maamuzi kwa kutumia taarifa sahihi badala ya hisia za muda mfupi.

## Pitia uwekezaji wako mara kwa mara

Uwekezaji si jambo la kufanya mara moja na kulisahau kabisa.

Ni muhimu kuupitia mara kwa mara ili kuona kama bado unaendana na malengo yako. Mahitaji ya maisha hubadilika kadiri miaka inavyopita. Ndoa, watoto, biashara mpya au maandalizi ya kustaafu vinaweza kuhitaji marekebisho ya mpango wako wa uwekezaji.

Pia ni muhimu kuendelea kujifunza kwa sababu mazingira ya biashara na uwekezaji hubadilika kila wakati.

Kwa kuhitimisha, niseme uwekezaji si safari ya siku moja wala si shughuli ya matajiri pekee. Ni mchakato unaohitaji maandalizi, elimu na subira. Kwa kujenga msingi mzuri wa kifedha, kuweka malengo wazi, kujifunza kanuni za uwekezaji na kuchagua fursa zinazokubalika kisheria na kidini, mtu anaweza kujenga ustawi wa kifedha hatua kwa hatua.

Katika Uislamu, mali ni amana kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hivyo, kuwekeza kwa busara si tu njia ya kutafuta faida, bali pia ni sehemu ya kutumia neema hiyo kwa uwajibikaji na kwa manufaa ya familia na jamii.

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

# Tujitathmini tunapouanza Mwaka Mpya wa 1448 Hijriya

Wiki hii inahitimisha mwaka wa Kiislamu 1447 na kuanza rasmi Mwaka Mpya wa 1448 Hijriya. Tuna wajibu wa kumshukuru Allah kwa neema zake alizotujaalia katika kipindi chote cha mwaka uliopita.

Kuingia kwa Mwaka Mpya wa 1448 si tukio la kubadilika kwa tarehe pekee, bali ni mwito kwa kila Muislamu kutafakari safari yake ya maisha na kujiuliza kama amepiga hatua kuelekea kuwa mja bora zaidi mbele ya Allah na mwanajamii mwema zaidi.

Hivyo, tunapaswa kujitathmini, kujikosoa na kupanga upya maisha yetu kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu pamoja na maadili mema ya kibinadamu.

Mwaka Mpya wa Hijriya ni fursa muhimu ya kuweka malengo makubwa yenye manufaa kwa dini, jamii, familia na taifa. Ni wakati wa kutafakari utendaji wetu ili kubaini tulikojikwaa, tulikofanikiwa na namna tutakavyosonga mbele.

Tutakuwa tunafanya kosa kubwa ikiwa miaka inaendelea kuyoyoma huku matendo, maamuzi na fikra zetu vikibaki vilevile.

Kama watu wenye shauku ya kupata mafanikio katika dini na dunia, ni vyema tukajitazama kwa jicho la tafakuri na kujiuliza: Je, tumeimarika kiimani? Je, tumetimiza wajibu wetu kwa Allah, familia zetu na jamii kwa ujumla? Mwaka uliopita umeacha alama gani katika maisha yetu? Maswali haya hayapaswi kututisha, bali yanapaswa kutuchochea kufanya mageuzi chanya.

Wenye akili ni wale wanaojichunguza wenyewe, kujilaumu kwa dosari zao na kisha kurekebisha mwenendo wao. Kutojichunguza si jambo jema kwa



Muislamu.

Kwa waliokufuru, wamejitafutia upotofu wenyewe kwa sababu hawafikiri kwamba kuna anayewaangalia. Allah Mtukufu anasema: "Hakika wao walikuwa hawataraji kuhesabiwa." [Qur'an, 78:27].

Tunapouanza Mwaka Mpya wa Hijriya, tuna dhima na wajibu wa kutafuta suluhu ya kudumu kwa changamoto mbalimbali zinazoendelea kujitokeza katika jamii zetu, ikiwamo mmomonyoko wa maadili, ongezeko la migogoro ya kifamilia, uzembe kazini pamoja na kupungua kwa mshikamano wa kidini na kijamii.

Haya yote yanahitaji marekebisho ya kina yanayoanzia kwa mtu mmoja mmoja. Mabadiliko ya kweli huanzia moyoni kabla ya kuonekana katika jamii.

## Toba, suluhu na amani

Mwaka 1447 Hijriya umeondoka na matendo yetu, ambayo tutaoneshwa Siku ya Ufufuo. Allah anasema: "Siku hiyo (ya Kiyama) mtu ataambiwa yale aliyoyatanguliza na yale aliyoyaahirisha." [Qur'an, 75:13]. Hivyo basi, hatuna budi kutubia kwa Allah, kumuomba msamaha na kujipanga kutenda mema zaidi.

Kwa upande mwingine, Mwaka Mpya wa 1448 unatupa fursa ya kuimarisha uhusiano wetu na watu wengine, kudumisha amani, kusameheana na kuacha chuki pamoja na visasi. Hakuna mkamilifu miongoni mwetu, na kila mmoja ana dosari zake.

Kwa upande wa maendeleo binafsi, tunapaswa kujitahidi kuongeza elimu, hususan elimu ya dini, kuboresha afya zetu, na kufanya kazi kwa bidii, weledi na uaminifu.

Uislamu unahimiza juhudi, uwajibikaji na uzalendo, hivyo ni muhimu kuyatafuta mafanikio ya kidunia sambamba na mafanikio ya Akhera. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kuimarisha Uislamu na kuchangia maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

Tusiuone mwaka mpya kama mzunguko wa kawaida wa kalenda, bali kama mwito wa kufanya mabadiliko ya kweli. Tujitathmini, tujirekebishe na tuanze ukurasa mpya wa maisha kwa matendo mema, nia njema na juhudi za dhati.

Tunapaswa kuendesha shughuli zetu kwa njia inayochangia maendeleo na ustawi wa Uislamu, huku tukihakikisha kwamba ibada zetu zinakuwa daraja la kutuimarisha kiroho na kutusogeza karibu zaidi na Muumba wetu.

Ibada zetu zisibaki kuwa mazoea ya kila siku yanayotekelezwa bila tafakuri, bali ziwe chachu ya mabadiliko chanya katika maisha yetu binafsi na ya jamii kwa ujumla. Ni kwa kufanya hivyo ndipo mwaka mpya wa Hijriya utakuwa na maana katika maisha yetu.

# Nini baada ya Hijja?

## Tumejifunza nini kutoka katika Ihram?

**Katika makala iliyopita tuliona kwamba Hijja si mwisho wa safari ya kiroho bali ni mwanzo wa mabadiliko mapya katika maisha ya Muislamu. Tulihitimisha kwa kujiuliza kuhusu hatua ya kwanza kabisa ya safari hiyo adhimu; hatua ambayo kila hujaji analazimika kuipitia kabla ya kuingia katika matendo makubwa ya hijja. Hatua hiyo ni Ihram.**

**Kwa mtazamo wa wengi, Ihram ni vazi maalumu linalovaliwa wakati wa Hijja au Umrah. Lakini kwa hakika, Ihram ni zaidi ya mavazi.**

**Ihram ni somo kubwa la maisha, ni tangazo la kuingia katika hali ya utiifu maalumu kwa Mwenyezi Mungu, na ni mwanzo wa malezi ya kiroho ambayo hujaji anatakiwa kuyaishi hata baada ya kurejea nyumbani.**

### Safari inaanza kwa kuvua tofauti zetu

Moja ya mambo ya kwanza yanayomgusa mtu anapoingia katika Ihram ni kuvua mavazi yake ya kawaida. Tajiri huacha mavazi yake ya thamani, kiongozi huacha alama za mamlaka yake, na mwenye cheo huacha ishara za hadhi yake. Wote huvaa mavazi yanayofanana.

Ni kana kwamba Hijja inamwambia mwanadamu: "Kabla ya kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu, acha kwanza yale yote yanayokutofautisha na wengine."

Katika maisha ya kawaida watu hutofautishwa kwa mali, elimu, vyeo, makabila na mataifa yao. Lakini ndani ya Ihram tofauti hizo hupotea. Kila mmoja huwa mja wa Mwenyezi Mungu, anayehitaji rehema na msamaha Wake.

Hili ni fundisho ambalo ulimwengu wa leo unalihitaji sana. Jamii nyingi zimegawanyika kwa misingi ya rangi, ukabila, utaifa na maslahi binafsi. Ihram humfundisha Muislamu kwamba heshima ya kweli haipatikani kwa mambo hayo, bali kwa ucha-Mungu.

### Somo la Unyenyekevu

Hakuna anayefika katika Hijja isipokuwa anagundua udogo wake mbele ya ukuu wa Mwenyezi Mungu.

Katika Ihram, mtu huacha mapambo mengi aliyoyazoea. Huvaa mavazi mepesi yasiyoonesha fahari wala utukufu wa kidunia. Hali hiyo humkumbusha kuwa mwanadamu, licha ya mafanikio yote anayoweza kuyapata duniani, bado ni mja dhaifu anayemhitaji Mola wake Mlezi kila wakati.

Tatizo kubwa la mwanadamu mara nyingi si umaskini wa mali, bali ni kiburi cha nafsi. Watu wengi huangamia kwa sababu ya kujiona bora kuliko wengine. Ihram huja kuvunja kiburi hicho na kumfundisha Muislamu kuwa heshima yake ya kweli iko katika utiifu wake kwa Mwenyezi Mungu.

### Nidhamu ya Nafsi

Anapoingia katika Ihram, hujaji huwekewa mipaka maalumu ambayo kwa kawaida haikuwepo katika maisha yake ya kawaida.

Haya ni mafunzo muhimu sana. Muislamu anafundishwa kwamba uhuru wa kweli haupatikani kwa kufanya kila unachokitaka, bali kwa kuweza kuizuia nafsi yako inapohitaji jambo ambalo Mwenyezi Mungu amelipiga marufuku.

Nafsi inayoweza kujidhibiti katika Ihram ndiyo inayoweza kujidhibiti pia baada ya hijja.

Ikiwa mtu aliweza kujiepusha na mambo yaliyoruhusiwa hapo awali kwa sababu ya amri ya Mwenyezi Mungu, basi anapaswa kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kujiepusha na mambo ambayo tayari ni haramu katika maisha yake ya kila siku.

### Kumbukumbu ya safari ya mwisho

Wanazuoni wengi wameeleza kuwa miongoni mwa hekima za Ihram ni kumkumbusha mwanadamu kuhusu mwisho wake.

Mtu anapoangalia umati mkubwa wa mahujaji waliovaa mavazi yanayofanana, hawezi kukosa kukumbuka siku ambayo wanadamu watakusanywa mbele ya Mola wao Mlezi.

Kumbukumbu hiyo humsaidia Muislamu kutathmini maisha yake. Humkumbusha kuwa dunia ni ya muda mfupi na kwamba safari ya mwisho ni kuelekea kwa Mwenyezi Mungu.

Mtu anayeikumbuka Akhera huwa mwangalifu zaidi katika matendo yake, maneno yake na mahusiano yake na watu wengine.

### Je, tunabaki na nini baada ya kuvua Ihram?

Baada ya kukamilika kwa ibada za hijja, hujaji huvua Ihram. Lakini swali muhimu ni hili: Je, mafunzo ya Ihram nayo yavuliwe pamoja na mavazi hayo?

Jibu ni hapana. Mavazi ya Ihram huondolewa, lakini unyenyekevu unabaki. Masharti ya Ihram huisha, lakini nidhamu ya nafsi inaendelea.

Mkusanyiko wa mahujaji hutawanyika, lakini somo la usawa wa wanadamu linapaswa kubaki moyoni. Haya ndiyo matunda ya kweli ambayo Muislamu anatakiwa kuyabeba baada ya hijja.

### Hitimisho

Ihram ni somo la kwanza katika shule ya hijja. Ndani yake Muislamu hujifunza usawa, unyenyekevu, nidhamu na kumbukumbu ya Akhera. Ni somo linalomwandaa kwa hatua zinazofuata za safari yake ya kiroho.

Lakini pamoja na mafunzo hayo yote, kuna lengo kuu ambalo Hijja imekusudiwa kulijenga ndani ya moyo wa Muislamu. Lengo hilo ndilo lililotajwa mara nyingi ndani ya Qur'an, na ndilo kipimo cha ubora wa mwanadamu mbele ya Mwenyezi Mungu.

Lengo hilo ni Taqwa.

Je, Hijja inamjengaje Muislamu kuwa mcha-Mungu? Kwa nini Qur'an imeunganisha ibada nyingi na ucha-Mungu? Na ni kwa namna gani hujaji anaweza kuhifadhi Taqwa baada ya kurejea katika maisha yake ya kawaida?

Hijja ni Shule ya Ucha-Mungu ndiyo tutakayoyachambua katika sehemu ijayo ya mfululizo huu.

*Itaendelea...*

ذو الحجة

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 1

Na Said Rajab
0783 650 803

# Miaka 78 baada ya Nakba, nini kinafuata?



Nakba (Msiba Mkuu) ni neno ambalo kila linapotajwa huibua katika fikra za Waislamu duniani kote suala la Palestina.

Mwaka 1948, Mazayuni walivamia Palestina, wakawafukuza wakazi wake kutoka katika ardhi zao na kumwaga damu kwa kuwaua wanawake, wanaume, watoto, vijana na wazee, huku wakisababisha uharibifu mkubwa.

Mataifa ya Kiarabu yalipopokea taarifa hizo, Jordan, Iraq, Misri, Lebanon na Syria zilihamasisha majeshi yao kuelekea Palestina. Mapigano dhidi ya wavamizi wa Kizayuni yalikuwa makali, huku askari wa majeshi hayo wakipigana kutoka pande mbalimbali hadi vilio vya Mazayuni vikafika katika nchi za Magharibi kupitia Umoja wa Mataifa. Hapo ndipo usaliti ulipoanza.

Pande zilizokuwa zikipigana dhidi ya Mazayuni zilikubaliana kusitisha mapigano kwa muda wa mwezi mmoja kwa kile kilichoelezwa kuwa misingi ya kibinadamu.

Unaweza kujiuliza: Je, majeshi ya nchi za Kiarabu yaliwezaje kukubali makubaliano hayo wakati yalikuwa yakishinda vita na yalikaribia kuwaangamiza Mazayuni? Jambo la kushangaza zaidi ni kwamba kamanda wa Jeshi la Waarabu kutoka Jordan, John Bagot Glubb (Glubb Pasha) alikuwa afisa wa Uingereza.

Aidha, makamanda wengine wa majeshi ya Kiarabu pamoja na viongozi wa nchi zao walitoa amri za kujiondoa katika maeneo fulani, licha ya kuwa walikuwa wakishinda mapigano katika maeneo hayo.

Hali hiyo ilitokea huku wakijua wazi kuwa jukumu lao la msingi lilikuwa kusonga mbele kumkabili adui, na si kurudi nyuma. Kabla ya muda wa makubaliano ya kusitisha mapigano kumalizika, Mazayuni walikiuka makubaliano hayo.

Kwa siku 26 mfululizo, vifaa vya kijeshi kutoka nchi za Magharibi vilipelekwa kwao, jambo lililowawezesha kuzingira na kupambana kwa ufanisi dhidi ya majeshi ya Kiarabu na hatimaye kuyalazimisha kuondoka.

Kadri miaka ilivyopita, mwaka 1964 Chama cha Ukombozi wa Palestina (PLO) kilitangazwa nchini Misri kuwa mwakilishi rasmi wa Wapalestina.

Inaonekana kuwa lengo la ndani la chama hicho lilikuwa kukabidhi ardhi iliyobaki ya Palestina kwa wavamizi, na hivyo kuhalalisha jambo ambalo nchi za Kiarabu zililikataa na hata kuamua kupeleka majeshi yao Palestina.

Sababu ya mtazamo huo ni kwamba moja ya mafanikio makubwa ya PLO ilikuwa kusaini Makubaliano ya Oslo, yaliyotambua uwepo wa dola ya Kizayuni katika asilimia 78 ya ardhi ya Palestina, huku asilimia 22 iliyobaki ikiachwa kwa mazungumzo.

Kati ya asilimia hiyo 22, ni asilimia 14 pekee ndiyo iliyobaki mikononi mwa Wapalestina kwa sasa. Hali hiyo imechagizwa na kuundwa kwa Mamlaka ya Palestina kupitia Makubaliano ya Oslo, ambayo hata hivyo yamekuwa yakikosolewa kwa madai ya kuwa na hila nyingi.

Rais wa Mamlaka ya Palestina, Mahmoud Abbas aliwahi kuyaelezea Makubaliano ya Oslo kuwa ni "uhaini" wakati wa hotuba yake katika Mkutano Mkuu wa Nane wa Fatah. Hata hivyo, alisisitiza kuwa, "Makubaliano ya Oslo ni usaliti, lakini tunayataka... tunataka kuyahifadhi."

Kauli hiyo inazua swali muhimu: je, kuna mantiki gani ya kuhifadhi makubaliano yanayoelezwa kuwa ni ya usaliti? Zaidi ya miaka 32 tangu kusainiwa kwa makubaliano hayo, hakuna mabadiliko yoyote yaliyoonekana katika vitendo vya Mazayuni dhidi ya Wapalestina.

Mauaji ya raia yanaendelea, Wapalestina wanafurushwa kutoka katika maeneo yao, wanawekewa mizingiro, nyumba zao zinabomolewa na wengi wao hukamatwa kiholela.

Kwa hakika, dola ya Kizayuni imeongeza mashambulizi yake katika maeneo Matakatifu ya Waislamu huko Jerusalem, Al–Khalil na sehemu nyingine.

ذو الحجة فتاوى



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Hijja ya mwanamke inasihi bila kuwa na mahram?

**Swali: Je, ni kweli kwamba mwanamke anatakiwa kuwa na mahram ili Hijja yake iwe sahihi? Na ikiwa hana mahram, si wajibu kwake kuhiji?**

**Jibu:** Ndiyo, kuna hadith sahihi iliyopokewa na Abdullah bin Abbas kwamba Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Mwanamke asisafiri isipokuwa akiwa na mahram wake."

Kisha kuna mtu mmoja akasema: "Ewe Mtume wa Allah, mke wangu ametoka kwenda kuhiji, na mimi nimeandikishwa kwenda katika vita fulani." Mtume (Allah amshushie rehema na amani) akamwambia: "Nenda ukahiji pamoja na mke wako." [Bukhari na Muslim].

Hata hivyo, wanazuoni wamekhitilafiana kuhusu je, mahram ni sharti la kuswihi kwa hijja. Zipo kauli tatu.

## Kauli ya kwanza

Wanazuoni wengi, miongoni mwao Ahmad bin Hanbal na wengine katika madhehebu yake wamesema mahram ni sharti la uwajibu wa Hijja kwa mwanamke. Ikiwa hana mahram, Hijja haimlazimu mpaka apate mahram. Akisafiri bila mahram atakuwa ametenda kosa lakini Hijja yenyewe ikitimiza nguzo na masharti yake huswihi.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa kauli hii, si sahihi kusema Hijja yake ni batili bali anakuwa amefanya safari isiyoruhusiwa.

## Kauli ya pili

Baadhi ya wanazuoni wa madhehebu ya Shafi'i na Malik wanasema kwamba mwanamke anaweza kwenda Hijja ya faradhi bila mahram, ikiwa kuna usalama wa kutosha na anaambatana na kundi la watu waaminifu. Wanategemea dalili nyingine na pia mazingira ya usalama.

## Kauli ya tatu

Baadhi ya wanazuoni wa zama za karibuni wameona kwamba ikiwa usalama umehakikishwa kupitia misafara rasmi ya hijja, usafiri wa ndege, na taratibu za serikali; basi mwanamke anaweza kwenda kutekeleza Hijja ya faradhi hata bila mahram.

## Ni ipi kauli yenye nguvu zaidi?

Wanazuoni wengi wa zamani waliona kwamba hadithi za katazo la mwanamke kusafiri bila mahram ni za wazi na za jumla, hivyo mahram ni sharti kwa mwanamke katika safari ya Hijja na safari nyinginezo. Hii ndiyo kauli iliyochukuliwa na wanazuoni kama Abdul-Aziz bin Baz na Muhammad bin Swaleh al-Uthaymeen.

Kwa mujibu wa kauli hii mwanamke asiye na mahram bado hajalazimikiwa Hijja mpaka apate mahram.

Akihiji bila mahram, Hijja yake huswihi ikiwa amekamilisha nguzo na wajibu wa hijja, lakini anakuwa ametenda dhambi ya kusafiri bila mahram.

Hivyo, hadith ipo na ni sahihi, lakini kusema kwamba "Hijja ya mwanamke bila mahram haiswihi kabisa", si jambo ambalo wanazuoni wote wamelikubali. Wengi wao hutofautisha kati ya kuswihi kwa Hijja na kuruhusiwa kwa safari. Hijja inaweza kuswihi, huku safari yenyewe ikawa imefanyika kwa namna isiyoruhusiwa kwa mujibu wa kauli yao. Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Wanazuoni wanamzunguziaje kuhusu kuwapokea mahujaji, kusifiwa au kujisifu kwa Hijja na kujiita Al-haji?**

**Jibu:** Kwa ufupi, masuala haya yamezungumziwa na wanazuoni kama Muhammad bin Swaleh al-Uthaymin na Abdul-Aziz bin Baz katika muktadha wa nia, kujiepusha na riyaa (kujionesha), na kufuata Sunna.

## Kuwapokea mahujaji wanaporudi kutoka hijja

Wanazuoni wameeleza kuwa kuwapokea mahujaji ni jambo linaloruhusiwa na lina asili katika Sunna. Imepokewa kuwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa akipokelewa aliporudi kutoka safari na maswahaba walikuwa wakikutana na wasafiri waliorejea. Hata hivyo, haya yasifanyike kwa kujifakharisha au kufanya sherehe zenye israfu. Wala isihusishwe na itikadi kwamba ni ibada maalumu yenye thawabu maalumu isipokuwa kwa dalili. Kubadilishana pongezi na kumuombea Hijja yake ikubaliwe ni jambo jema.

## Kusifiwa kwa kufanya hijja

Ikiwa watu wanamsifu mtu kwa kuwa amehiji bila yeye kutafuta sifa hizo, hakuna ubaya. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliita sifa njema za watu kwa Muumini kuwa ni "bishara ya haraka kwa Muumini".

Lakini, hujaji anatakiwa kujihadhari na kujivuna au kufurahia sifa kwa namna ya kiburi. Lengo la Hijja ni kupata ridhaa za Allah, si kupata heshima ya watu.

## Kujisifu kwa hijja

Wanazuoni wameonya dhidi ya mtu kuifanya Hijja kuwa sababu ya kujitukuza mbele ya watu, kama kusema: "Mimi ni Haji, nyinyi hamjahiji," au kujiona bora kuliko wengine kwa sababu ya hijja.

Hili linaweza kuharibu ikhlasi na kupunguza athari za ibada hiyo. Kuhusu kuitwa au kujiita "Alhajj" kwa mujibu wa fatwa za wanazuoni wengi akiwemo Sheikh Ibn Baaz na Sheikh Ibn Uthaymin, hakuna ubaya ikiwa ni kwa maana ya kumtambua kwamba ameshahiji. Lakini si Sunna kufanya hilo kuwa cheo cha kidini kinachotangulizwa kila mara mbele ya jina.

ذُو الحِجّة

# NASAHA ZA WIKI

0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Hasara ilioje kupuuza ibada kisa Kombe la Dunia



Alhamisi ya Juni 11 mwaka huu, pazia la michuano ya soka ya Kombe la Dunia lilifunguliwa huko Mexico City nchini Mexico, ambapo mataifa 48 yanawania kutwaa ubingwa wa dunia.

Ni kawaida kila unapowadia msimu wa Kombe la Dunia kuona mashabiki wa soka wakiwa 'bize' kufuatilia michuano hiyo hatua kwa hatua.

Kwa sababu ya kupenda sana soka, Waislamu wengi pia wamekuwa wakijishughulisha na kutazama michuano hiyo kupitia runinga, kiasi cha kuwafanya waache ibada za sala, dhikri, kusoma Qur'an na majukumu mengine ya wajibu.

Ukichunguza katika misikiti mingi ya mijini (siyo yote), utaona kuwa idadi ya waumini hupungua pindi ratiba za mechi zinapogongana na muda wa sala.

Hii inaonesha namna wanadamu walivyotekwa na anasa za dunia, ambazo lengo lake hasa ni kupumbaza akili. Ni wazi kuwa imani za baadhi yetu zina kasoro kutokana na kupenda sana mambo ya anasa na starehe.

Wengi tunapenda vitu mbalimbali vya kidunia, ukiwamo mpira wa miguu, kuliko tunavyompenda Allah, Mtume wake na Uislamu wetu.

Iblis (shetani aliyelaaniwa) ameupamba mchezo wa soka kiasi cha kuufanya kuwa kipenzi zaidi kwetu kuliko Allah na Mtume wake. Kibaya zaidi, nyoyo zetu zimekuwa ngumu kama mawe, au hata zaidi ya mawe linapokuja suala la kufuatilia soka.

## Michezo katika Uislamu

Kucheza michezo ya kujenga mwili ni jambo lililoruhusiwa na kuhimizwa sana katika Uislamu. Hata hivyo, kuna sheria na kanuni zinazotawala michezo katika Uislamu, ambazo wengi hawazifahamu, na hata wanaozifahamu hawazizingatii.

Ipo baadhi ya michezo ambayo, kwa sababu fulani imeharamishwa. Mfano ni mchezo wa masumbwi, ambapo watu wawili hukabiliana ulingoni wakipigana ngumi. Mchezo huo ni haramu moja kwa moja.

Uharamu wake unatokana na washindani wawili kupigana ngumi hadi kufikia kuumizana na damu kutoka, au hata wengine kufa kwa kipigo.

## Soka linavyopotosha watu

Iblis alipolaaniwa na kufukuzwa katika rehema za Allah Ta'ala aliapa kwa kusema: "... Mola wangu Mlezi! Kwa kuwa umenihukumu kupotea, bila shaka nitawapambia (maasi) katika ardhi na nitawapotosha wote." [Qur'an, 15:39].

Madhara ya soka kisaikolojia ni makubwa mno. Kwanza, mashabiki wa soka hupata presha na kukosa utulivu pindi timu zao zinapocheza.

Pili, mchezo wa soka siku hizi unahusishwa na mambo mengi ya haramu kama ulevi na kamari, mambo ambayo yanapingana na maadili ya Kiislamu yanayohimiza kujiepusha na haramu na mali inayopatikana kwa njia zisizo halali.

Aidha, soka huwafanya watu wasihifadhi Qur'an na adhkari mbalimbali kwa kuwa hutumia muda wao mwingi kuhifadhi majina ya wachezaji wa timu zao.

Leo hii, ukimwambia Muislamu anayeshabikia soka akutajie kikosi cha wachezaji 11 wa timu anayoipenda waliocheza michuano fulani, hata kama ni mwaka 1990, atakutajia mmoja baada ya mwingine.

Lakini muulize jambo la msingi katika Uislamu umsikie atakavyong'aka: "Wewe vipi, unanifanya mjinga? Unadhani mimi sijui?" Yote hayo ni kukwepa tu kwa sababu akili imeshapumbazwa na soka.

Muulize nguzo za dini ni ngapi, au nguzo za swala, au mambo yanayoharibu swaumu, uone kama atakujibu.

Katika Uislamu kuna kanuni inayoitwa 'Al–Walaa Wal–Baraa', yaani kupendana kwa ajili ya Allah na kuchukiana kwa ajili ya Allah.

Ukifanya utafiti mdogo utabaini kuwa wengi wetu tunawapenda mno wanasoka, wasanii wa muziki na filamu, jambo ambalo linakinzana na kanuni hii ya 'Al–Walaa Wal–Baraa'. Muislamu anatakiwa awapende zaidi Waislamu wenzake, kwa kuwa hiyo ni sifa mojawapo ya waumini wa kweli.

## Maswahaba walimpenda zaidi Allah na Mtume wake

Miaka zaidi ya 1,500 iliyopita, ulimwengu ulikuwa katika giza la ujahili na maovu. Watu walikuwa wakitafuta msuluhishi ambaye angerekebisha itikadi na maadili ya watu.



MAKALA MAALUM

SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811



# Haki ya kumhudumia mke katika ndoa



Sharia ya Kiislamu ilikuja katika kipindi ambacho watu walikuwa wakitawaliwa na sheria za ukandamizaji. Mwanamke alinyanyaswa na hakuhesabiwa kuwa binadamu kamili sawa na mwanaume.

Mwanamke alikuwa akirithiwa pamoja na mali nyingine za marehemu. Aidha, baadhi ya watoto wa kike walikuwa wakizikwa wakiwa hai katika umri mdogo. Hili limeelezwa wazi ndani ya Qur'an pale Allah Mtukufu aliposema: "Na mtoto wa kike aliyezikwa akiwa hai atakapoulizwa; Kwa dhambi gani aliuawa?" [Qur'an, 81:8–9].

Kwa ajili hiyo, Uislamu ukampa mwanamke haki zake na kuthibitisha kuwa ana haki pamoja na wajibu unaowiana na wa mwanaume. Allah anasema: "...nao (wanawake) wana haki zinazolingana na wajibu wao kwa mujibu wa mema." [Qur'an, 2:228].

Uislamu unamheshimu mwanamke katika nafasi zake zote; iwe ni mama, dada, binti au mke. Aidha, umempa hadhi ya kutunzwa na kugharamiwa na mume wake.

Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie) amesisitiza hilo aliposema: "Nyinyi mnawajibika kuwapa wake zenu riziki yao na mavazi yao kwa njia inayofaa." Hayo yote yanaonesha jinsi Uislamu unavyomjali, kumheshimu na kumlinda mwanamke, kinyume na madai ya wale wanaouchukia Uislamu.

Wanazuoni wa Sharia ya Kiislamu (Fuqahau) wameeleza maana ya kumhudumia mke kuwa ni kumpa kila anachohitaji katika chakula, makazi, huduma na matibabu, hata kama ni tajiri.

Wapo waliosema kuwa kumhudumia mke ni kumpa chakula, kitoweo, mavazi na makazi kwa mujibu wa desturi ya watu. Kwa maana kwamba kiwango na aina ya chakula, kitoweo na mavazi hupimwa kwa kuzingatia desturi na hali iliyozoeleka katika jamii na mji wanaoishi wanandoa.

Wajibu huu wa kumhudumia mke umethibiti katika Qur'an pale Allah Mtukufu aliposema: "Wawekeni (wake zenu) kwenye nyumba mnazoishi kulingana na uwezo wenu, wala msiwadhuru kwa kuwabana." [Qur'an, 65:6].

Aya hii inaonesha wajibu wa mume kumpatia mkewe nyumba ya kuishi. Na unapothibiti wajibu wa makazi, basi pia huthibiti wajibu wa chakula, mavazi na mahitaji mengine ya msingi ya maisha.

Pia kuna hadith nyingi za Mtume zinazoonesha wajibu wa kumhudumia mke, ikiwamo hadith ya Hind bint Utba (Allah amridhie), ambaye alimlalamikia Mtume (rehema na amani zimshukie) kuhusu mumewe (Abu Sufyan) kuwa ni bahili sana na hatoi matumizi ya kutosha kwa ajili yake na watoto wake.

Mtume alimruhusu Hind kuchukua mali kutoka kwa Abu Sufyan kiasi kinachomtosha yeye na wanawe, kwa njia ya haki na kwa mujibu wa ada, hata bila Abu Sufyan kufahamu.

Hadith hii ni ushahidi wa wazi kwamba mume ana wajibu wa kutoa matumizi kwa mkewe na watoto wake. Wanazuoni wamekubaliana kwamba ni wajibu wa mume kumgharamia mkewe katika mahitaji ya kila siku.

Hata hivyo, wametofautiana kuhusu sababu inayofanya wajibu huo uthibiti. Je, matumizi yanakuwa wajibu kwa sababu ya mke kumtii mumewe katika maisha ya ndoa, au yanakuwa wajibu mara tu mkataba sahihi wa ndoa unapofungwa?

Wanazuoni wa madhehebu ya Shafi wamesema kuwa kumhudumia mke ni wajibu pale mke anapojikabidhi kikamilifu kwa mume wake. Kwa mtazamo wao, matumizi hayathibiti kwa kufunga ndoa pekee.

Aidha, wanazuoni hao wameeleza kuwa haki ya mke ya kupata matumizi hupotea katika hali zifuatazo. Kwanza, mke anapotoka katika utiifu wa mume wake katika mambo ambayo sharia imempa mume haki. Pili, mke kutoka nyumbani bila ruhusa ya mumewe, hata kama kutoka kwake ni kwa ajili ya ibada au jambo jingine jema. Hata hivyo, ikiwa ana udhuru wa kisharia, akitoka hahesabiwi kuwa amefanya uasi.

Tatu, ikiwa mke ametoka nyumbani kutokana na kudhulumiwa, kuonewa au kupata madhara, kutoka kwake hakuhesabiwi kuwa ni uasi. Hivyo, anastahiki kuendelea kuhudumiwa kwa kuwa ametoka kwa haki na si kwa uasi.

Nne, ikiwa mume amefilisika au hana uwezo wa kutoa matumizi ya mkewe, basi matumizi hayo hubaki kuwa deni kwa mume.

Wanazuoni wa madhehebu ya Shafi wamegawa matumizi katika aina mbili. Mosi, matumizi ya mume mwenye uwezo (tajiri), na pili matumizi ya mume mwenye kipato cha kati au mwenye uwezo mdogo.

Wameegemeza hoja yao juu ya kauli ya Allah Mtukufu: "Mwenye uwezo atoe kwa kadiri ya uwezo wake, na mwenye uwezo mdogo atoe kadiri ya uwezo wake." [Qur'an, 2:236].


Wanazuoni hao wamefafanua kuwa kiasi cha matumizi kinapaswa kuzingatia hali ya wanawake wanaofanana na mke huyo katika jamii anayoishi. Kwa mfano, ikiwa wanawake wa hadhi yake kwa kawaida huwa na mtumishi wa kuwasaidia, basi gharama za mtumishi hujumuishwa katika matumizi yake.

Ikiwa desturi ya wanawake wa hali yake ni kuishi bila mtumishi, mume hatakuwa na wajibu wa kumletea mtumishi. Kiwango cha chini cha matumizi ni kile kinachotosheleza mahitaji yake ya kawaida.

UONGOZI UTAWALA

NA UKHTI FATIMA SS
0789 201 383

# ADKAR na Prosci: Njia ya kimfumo ya kusimamia mabadiliko katika taasisi




Katika mazingira ya sasa ya kazi, mabadiliko yamekuwa jambo la kawaida. Taasisi zinabadilisha mifumo ya teknolojia, taratibu za kazi, sera, na hata utamaduni wa shirika ili kuendana na mahitaji ya wakati.

Hata hivyo, changamoto kubwa si kuanzisha mabadiliko hayo, bali kuhakikisha yanakubalika na kutekelezwa kwa mafanikio na watu wanaohusika.

## Mabadiliko ya mtu mmoja

Wataalamu wa usimamizi wa mabadiliko wanaeleza kuwa mabadiliko ya kweli ya taasisi huanza kwa mabadiliko ya mtu mmoja mmoja.

Ikiwa wafanyakazi hawataelewa, kukubali na kutumia mabadiliko yanayopendekezwa, hata mpango bora zaidi unaweza kushindwa. Ndiyo maana taasisi nyingi duniani hutumia mifumo wa Prosci ADKAR ulioasisiwa na Jeff Hiatt katika miaka ya 1990s kwa ajili ya kusaidia watu kupitia safari ya mabadiliko.

ADKAR ni kifupi cha maneno matano ya Kiingereza: Awareness (Ufahamu), Desire (Utayari), Knowledge (Maarifa), Ability (Uwezo) na Reinforcement (Uimarishaji). Mfumo huu unalenga kuhakikisha kuwa kila mfanyakazi anapitia hatua zote muhimu zinazomwezesha kukubali na kuendeleza mabadiliko.

Hatua ya kwanza ni Awareness, yaani kujenga ufahamu kuhusu sababu za mabadiliko. Watu wanahitaji kuelewa kwa nini mabadiliko hayo ni muhimu na ni changamoto gani yanakusudia kutatua. Bila ufahamu huu, mara nyingi hujitokeza upinzani na mashaka.

Hatua ya pili ni Desire, ambayo ni hamasa au utayari wa kushiriki katika mabadiliko. Hata kama mtu anaelewa sababu za mabadiliko, bado anaweza kukosa nia ya kushiriki. Hivyo, viongozi na wasimamizi wanapaswa kuonyesha manufaa ya mabadiliko hayo kwa mtu binafsi na kwa taasisi kwa ujumla.

Baada ya hapo hufuata Knowledge, yaani kuwapa watu maarifa kuhusu jinsi ya kutekeleza mabadiliko hayo. Hii inaweza kufanyika kupitia mafunzo, warsha, miongozo ya kazi na ushauri wa kitaalamu.

Hatua ya nne ni Ability, ambayo ni uwezo wa kutumia maarifa hayo katika mazingira halisi ya kazi. Mara nyingi hatua hii huhitaji mazoezi, usaidizi wa karibu na muda wa kutosha ili watu waweze kuzoea njia mpya za kufanya kazi.

Hatimaye, kuna Reinforcement, yaani kuimarisha na kudumisha mabadiliko hayo. Hii inaweza kufanyika kwa kutambua mafanikio, kutoa mrejesho chanya na kuhakikisha mifumo ya taasisi inaendelea kuunga mkono mabadiliko yaliyofanyika.

## Mabadiliko kitaasisi

Ingawa ADKAR husaidia katika ngazi ya mtu mmoja mmoja, taasisi pia zinahitaji mfumo mpana wa kusimamia mabadiliko katika ngazi ya shirika lote. Hapa ndipo Prosci 3-Phase Process inapokuwa muhimu.

Mfumo huu una hatua tatu kuu. Hatua ya kwanza ni Prepare Approach (Kuandaa Mkakati). Lengo lake ni kuweka msingi imara wa mabadiliko kwa kubuni mkakati unaoendana na mahitaji ya taasisi, huku ukihakikisha uongozi wa juu unaunga mkono mabadiliko hayo.

Hatua ya pili ni Manage Change (Kusimamia Mabadiliko). Katika hatua hii, taasisi huandaa na kutekeleza mipango mbalimbali ya mawasiliano, mafunzo, ushirikishwaji wa wadau na usimamizi wa upinzani ili kuhakikisha watu wanapitia hatua za ADKAR kwa mafanikio.

Hatua ya tatu ni Sustain Outcomes (Kudumisha Matokeo). Lengo ni kuhakikisha manufaa yaliyotarajiwa yanapatikana na mabadiliko hayo yanakuwa sehemu ya kawaida ya utendaji wa taasisi. Hii inahusisha ufuatiliaji wa matokeo, tathmini ya maendeleo na kuimarisha tabia mpya za kazi.

Kwa ujumla, uzoefu wa taasisi nyingi duniani unaonyesha kuwa mafanikio ya mabadiliko hayategemei teknolojia, sera au bajeti pekee.

Mafanikio yanategemea uwezo wa kuwasaidia watu kubadilika. Mfumo wa ADKAR hutoa mwongozo wa mabadiliko kwa mtu mmoja mmoja, huku Prosci 3-Phase Process ukitoa mwongozo wa mabadiliko katika ngazi ya shirika. Kwa kuunganisha mifumo hii miwili, taasisi zinaweza kuongeza uwezekano wa kufanikisha mabadiliko na kupata matokeo endelevu kwa muda mrefu.

# TUJIFUNZE

## AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

ذو الحجة

Na Junaynat Ally Dama




# AI inavyoweza kuwa kikwazo kwa ukuaji wa akili ya mtoto

Mtoto wa miaka tisa anakaa mezani akifanya kazi ya hesabu. Baada ya dakika chache anakwama. Anafikiria, anafuta alichoandika, anajaribu tena na bado hapati jibu.

Mama yake anamtazama. Anaweza kufanya mojawapo ya mambo mawili. Anaweza kumpatia jibu ili amalize haraka. Au anaweza kumruhusu aendelee kupambana na tatizo hilo kwa muda.

Wazazi wengi huchagua njia ya kwanza kwa sababu wana nia njema. Hawapendi kuwaona watoto wao wakihangaika. Lakini wataalamu wa elimu na saikolojia wanaeleza kuwa mara nyingi ukuaji wa akili hutokea hasa katika nyakati hizo za mapambano.

Katika ulimwengu wa leo, watoto wamezoea kupata majibu kwa haraka. Simu za mkononi, intaneti na sasa akili bandia (AI) vinaweza kutoa suluhisho ndani ya sekunde chache. Hata hivyo, kuna jambo muhimu ambalo teknolojia haiwezi kutoa: ukuaji wa ubongo unaotokana na juhudi za kutatua tatizo.

Wataalamu hutumia neno "productive struggle" kuelezea hali ambayo mwanafunzi anakutana na changamoto inayomlazimisha kufikiri kwa kina kabla hajapata suluhisho. Ingawa hali hiyo inaweza kuonekana ya kukatisha tamaa kwa muda mfupi, ndiyo mazingira ambayo ubongo hujifunza zaidi.

Fikiria jinsi misuli ya mwili inavyokua. Mtu hawezi kuwa na nguvu kwa kutazama wengine wakifanya mazoezi. Misuli hukua inapokabiliwa na mzigo unaoifanya ifanye kazi zaidi. Ubongo nao hufanya kazi kwa namna inayofanana

Mtoto anapojaribu kutatua tatizo la hesabu, kuandika insha au kuelewa somo gumu, ubongo wake huunda na kuimarisha njia mpya za mawasiliano kati ya seli za neva. Kadiri anavyoendelea kufikiri na kujaribu, ndivyo uwezo wake wa kutatua matatizo unavyoongezeka.

Tatizo la kizazi hiki ni kwamba mara nyingi tunachukulia ugumu kama ishara ya kushindwa.

Mtoto akikwama kwenye kazi ya shule, tunakimbilia kumsaidia. Akichoka kufikiri, tunampa jibu. Akipata changamoto, tunajaribu kuiondoa.

Lakini wakati mwingine kile tunachokiita msaada kinaweza kuwa kikwazo kwa ukuaji wake.

Hii haimaanishi kuwa watoto waachwe wapambane peke yao bila msaada wowote. Kazi ya mzazi au mwalimu si kutoa majibu yote, bali kutoa mwongozo unaomsaidia mtoto kuyapata mwenyewe.

Kwa mfano, badala ya kusema, "Jibu ni hili," unaweza kuuliza, "Umejaribu njia gani?" au "Ni sehemu gani hasa imekushinda?"

Maswali kama haya humlazimisha mtoto kuendelea kufikiri.

Katika zama za AI, somo hili limekuwa muhimu zaidi kuliko wakati mwingine wowote. Akili bandia inaweza kutatua matatizo mengi kwa haraka kuliko binadamu. Lakini ikiwa mtoto atategemea AI kila anapokwama, anaweza kukosa kujenga uwezo ambao angeuhitaji katika maisha yake yote.

Uwezo wa kufikiri kwa kina, kuvumilia changamoto na kutafuta suluhisho haujengwi kwa kusoma majibu. Unajengwa kwa kuyatafuta.

Wataalamu wa elimu wanaeleza kuwa wanafunzi wanaokutana na changamoto zinazolingana na uwezo wao na kuzitatua kwa juhudi zao wenyewe huwa na kumbukumbu bora zaidi na uelewa wa muda mrefu kuliko wale wanaopewa majibu moja kwa moja.

Hii ndiyo sababu baadhi ya masomo tunayakumbuka kwa miaka mingi. Si kwa sababu yalikuwa rahisi, bali kwa sababu tulilazimika kuyafanyia kazi.

Kwa upande mwingine, majibu ya haraka mara nyingi husahaulika kwa haraka. Kwa hiyo, wakati mwingine jambo bora zaidi ambalo mzazi anaweza kufanya si kumwondolea mtoto tatizo. Ni kuwa karibu naye wakati analitatua.

Mruhusu afikiri. Mruhusu akosee. Mruhusu ajaribu tena. Bila shaka atachukua muda mrefu zaidi. Lakini katika mchakato huo atakuwa anajenga kitu cha thamani zaidi kuliko jibu sahihi. Atakuwa anajenga uwezo wa kufikiri.

Na katika dunia ambayo mashine zinaweza kutoa majibu kwa sekunde chache, uwezo huo unaweza kuwa moja ya zawadi muhimu zaidi ambayo tunaweza kuwapa watoto wetu.

ذوالحجة

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama



# Mazingira machafu, afya hatarini

Mtu anaposikia habari za mabadiliko ya tabianchi, ukataji miti au uchafuzi wa mazingira, mara nyingi huona ni mada zinazohusu wanasayansi, wanamazingira au viongozi wa serikali. Lakini ukweli ni kwamba suala la mazingira ni suala la afya pia.

Hewa tunayovuta, maji tunayokunywa, chakula tunachokula na mazingira tunamoishi vina uhusiano wa moja kwa moja na afya zetu. Ndiyo maana wataalamu wa afya duniani wanaonya kwamba uharibifu wa mazingira umegeuka kuwa moja ya vitisho vikubwa vya afya ya binadamu katika karne ya 21.

Katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu, Umoja wa Mataifa na Shirika la Afya Duniani (WHO) wametoa onyo kwamba madhara ya mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira si tatizo la kesho, bali ni tatizo linaloua watu leo.

## Hewa chafu inaua kimya kimya

Miongoni mwa athari kubwa za mazingira kwa afya ni uchafuzi wa hewa.

Kulingana na WHO, mamilioni ya watu duniani hufariki kila mwaka kutokana na magonjwa yanayohusishwa na hewa chafu. Uchafuzi huo huongeza hatari ya magonjwa ya moyo, kiharusi, saratani ya mapafu na magonjwa mbalimbali ya mfumo wa upumuaji.

Katika baadhi ya miji mikubwa duniani, viwango vya uchafuzi wa hewa vimefikia kiwango kinachoweka mamilioni ya watu katika hatari ya kiafya kila siku. Hata watoto wadogo, wazee na watu wenye magonjwa sugu ndiyo wanaobeba mzigo mkubwa zaidi wa madhara hayo.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres amesema dalili za janga la mazingira sasa zinaonekana wazi kupitia hewa iliyochafuliwa, ardhi iliyoharibiwa na mifumo ya ikolojia inayoporomoka. Athari hizo tayari zinadhuru afya za watu na kuhatarisha maisha yao.

## Joto kali linaongeza magonjwa na vifo

Miaka ya karibuni imekuwa miongoni mwa miaka yenye joto zaidi kuwahi kurekodiwa duniani.

Kadiri joto linavyoongezeka, ndivyo hatari za kiafya zinavyoongezeka pia. Mawimbi ya joto kali yanaweza kusababisha upungufu wa maji mwilini, matatizo ya moyo, uchovu mkali na hata vifo.

WHO imeonya kuwa ongezeko la mawimbi ya joto linaendelea kuongeza kiwango cha magonjwa na vifo katika maeneo mengi duniani. Watu wanaofanya kazi nje, wazee na wagonjwa huwa katika hatari kubwa zaidi. Mbali na madhara ya moja kwa moja, joto kali pia huathiri uzalishaji wa chakula na upatikanaji wa maji safi, hali inayoweza kusababisha matatizo mengine ya kiafya.

## Mafuriko na ukame huleta magonjwa

Mabadiliko ya tabianchi yameongeza matukio ya hali mbaya ya hewa kama mafuriko, ukame na dhoruba. Mafuriko yanaweza kuharibu miundombinu ya maji na usafi wa mazingira, jambo linaloongeza hatari ya magonjwa yanayoenezwa kupitia maji machafu kama kipindupindu na kuhara.

Kwa upande mwingine, ukame unaweza kusababisha uhaba wa maji salama na chakula. Hali hiyo huongeza utapiamlo, hasa kwa watoto, na kudhoofisha kinga ya mwili dhidi ya magonjwa.

WHO imeeleza kuwa majanga ya hali ya hewa pia huchochea kuenea kwa magonjwa yanayoenezwa na wadudu kama mbu, huku yakivuruga huduma za afya na ugavi wa dawa katika maeneo yaliyoathirika.

## Afya ya akili nayo inaathirika

Mara nyingi watu huzungumzia madhara ya mazingira kwa mwili pekee, lakini afya ya akili nayo huathirika.

Kupoteza makazi kutokana na mafuriko, kuharibika kwa mashamba kutokana na ukame au kupoteza chanzo cha kipato kutokana na uharibifu wa mazingira kunaweza kusababisha msongo wa mawazo, hofu na mfadhaiko.

WHO imeonya kuwa hatari kwa afya ya akili na ustawi wa kisaikolojia zinaongezeka kadiri athari za tabianchi zinavyozidi kuwa kubwa.

Kwa familia nyingi, majanga ya mazingira si habari za televisheni bali ni matukio yanayobadilisha maisha yao kabisa.

## Chakula na maji salama viko hatarini

Uharibifu wa mazingira pia unaathiri usalama wa chakula.

Ardhi inapoharibika, misitu kupotea na mifumo ya mvua kubadilika, uzalishaji wa mazao hupungua. Hali hiyo huongeza njaa na utapiamlo, hasa katika nchi zinazoendelea.

Nchini Nigeria, wataalamu wameonya kuwa uchafuzi wa mazingira, ukataji miti, uchimbaji holela wa madini na uchomaji gesi umechangia kuharibika kwa mashamba, kupungua kwa samaki na kuongezeka kwa magonjwa. Athari hizo zimezidisha umaskini, kupunguza uzalishaji na kuongeza gharama za afya.

## Kila mtu ana jukumu

Ingawa serikali na makampuni makubwa yana wajibu mkubwa wa kulinda mazingira, wananchi nao wana nafasi muhimu.

NA ZAHARANI BARAKA

# Mabadiliko yanayohitajika baada ya kuhiji

**Ibada ya Hijja imefaradhishwa kwa malengo mahsusi ya kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya Muislamu, ikiwa ni pamoja na kuimarisha uhusiano mwema wa kijamii kwa mujibu wa mafundisho ya dini.**
**Athari za Hijja zinapaswa kuonekana kwa hujaji tangu anaporejea kutoka Hijja, na kuendelea kujidhihirisha katika nyanja zote za maisha kupitia uhusiano wake na watu na mwenendo wake wa kila siku.**
**Ni muhimu kutafakari mafunzo yatokanayo na Hijja ili mahujaji wafikie malengo yaliyokusudiwa na ibada hii.**

## Manufaa makubwa ya Hijja

Mahujaji wanapaswa kutambua kuwa wamepata manufaa makubwa kupitia ibada ya Hijja, ikiwamo kusamehewa madhambi yao na kurejea katika usafi wa kiroho kama walivyokuwa siku walipozaliwa.

Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Mwenye kuhiji, kisha asiseme maneno machafu wala kutenda maasi, atarejea akiwa msafi wa dhambi kama siku aliyozaliwa na mama yake." [Bukhari na Muslim].

Hadith hii inaonesha ubora wa Hijja iliyokubaliwa, ambayo hufuta madhambi ya mja. Hivyo, baada ya kupata neema hiyo kubwa, hujaji anapaswa kutoyarejea maasi na kuendelea kuhifadhi usafi wa daftari lake la matendo.

## Malezi ya uchamungu

Mwenyezi Mungu anasema: "Na chukueni akiba; na hakika bora ya akiba ni uchamungu." [Qur'an, 2:197]. Aya hii imekuja katika muktadha wa mafunzo ya Hijja na imehitimishwa kwa kusisitiza uchamungu.

Hii inaonesha kuwa moja ya malengo makuu ya ibada ya Hijja ni kumuinua mja katika daraja ya uchamungu na kumjenga katika utiifu wa Mwenyezi Mungu kwa dhati.

## Kuboresha tabia njema

Watu wengi huzingatia ibada za kimwili kama sala na swaum, lakini wakati mwingine husahau umuhimu wa tabia njema. Si ajabu kumkuta mtu akifanya juhudi kubwa katika ibada, lakini ana kasoro nyingi katika maadili na uhusiano wake na watu wengine.

Hivyo, ibada ya Hijja inapaswa kuwa shule ya malezi ya tabia njema, marekebisho ya mwenendo wa maisha, pamoja na kuhifadhi na kuimarisha utambulisho wa Kiislamu.

Katika ibada ya Hijja hakuna ubaguzi wa rangi, taifa, lugha wala kabila. Waislamu wote huvaa ihramu na kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu kwa usawa.

Mwenyezi Mungu anasema: "Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanaume na mwanamke, na tumekufanyeni kuwa mataifa na makabila (mbalimbali) ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule aliye mchamungu zaidi." [Qur'an, 49:13].

## Kuepuka mabishano yasiyo na faida

Mwenyezi Mungu anasema: "Wala hakuna mabishano katika Hijja." [Qur'an, 2:197]. Hata hivyo, baadhi ya watu wameyafanya mabishano kuwa njia yao ya kuelimishia wengine.

Badala ya kufundisha kwa hekima na kutoa mwongozo sahihi, hujihusisha na mijadala inayochochea ushindani wa hoja na kung'ang'ania misimamo binafsi.

Mazingira ya Hijja humfanya hujaji atende mambo kwa msingi wa elimu, maarifa na hekima. Aidha, humfundisha kuepuka mabishano yasiyo na manufaa – iwe katika masuala ya dini au mambo mengine ya maisha.

## Kuimarisha Tauhidi

Jambo muhimu zaidi kwa waliohiji ni kuimarisha tauhidi, yaani kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika ibada. Hili lilionekana wazi katika talbiya, takbiri na dua mbalimbali za Hijja.

Vitendo vyote hivyo vinathibitisha kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kujiepusha na shirk katika aina zake zote.

## Kutukuza alama za Mwenyezi Mungu

Mwenyezi Mungu anasema: "Na anayezitukuza alama za Allah, basi hilo ni katika uchamungu wa nyoyo." [Qur'an, 22:32]. Aya hii inaonesha umuhimu wa kuheshimu na kutukuza alama na ibada zilizowekwa na Mwenyezi Mungu, jambo ambalo ni dalili ya uchamungu wa kweli.

Hivyo, baada ya kutekeleza ibada ya Hijja, mahujaji wanapaswa kushikamana na tauhidi na kujiepusha na shirk. Hawapaswi kumuomba yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu, wala kuchinja, kuweka nadhiri, au kufanya ibada yoyote isipokuwa kwa ajili yake.

Vilevile, wanapaswa kuepuka kwenda kwa wachawi na makuhani au kuwaamini. Aidha, hawapaswi kutafuta baraka kwa njia ambazo hazijathibiti katika mafundisho ya Kiislamu.

## Kutubia na kuanza ukurasa mpya

Mahujaji wanapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajaalia kutekeleza ibada ya Hijja. Shukrani ya kweli ni ile inayoonekana kwa ulimi, moyo na vitendo.

Miongoni mwa shukrani hizo ni kuendelea kufanya mema, kuacha maovu na kuwalingania wengine katika kheri walizojifunza wakati wa Hijja, kama vile tauhidi, Ikhlas, uchamungu na tabia njema.

Kudumu katika mema mpaka mwisho wa uhai

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Njia za kumhamasisha kijana wako barobaro



Wazazi wengi hukutana na changamoto ya kuona watoto wao wa rika la ubarobaro wakikosa hamasa ya kusoma, kufanya kazi za nyumbani au kutekeleza majukumu mengine ya kila siku. Wakati mwingine kijana huonekana mzembe, mbishi au asiyejali, lakini ukweli ni kwamba mara nyingi vijana hawakosi hamasa kabisa; wanakosa hamasa ya kufanya yale ambayo watu wazima wanataka wafanye.

Kijana huyo huyo anayeonekana hana ari ya kusoma anaweza kutumia muda mrefu kwenye simu, michezo, marafiki, au jambo analolipenda. Hii inaonyesha kuwa uwezo wa kuhamasika upo. Changamoto ni namna ya kuuelekeza uwezo huo kwenye mambo yenye manufaa kwa maisha yake.

Kipindi cha ubarobaro huambatana na mabadiliko mengi ya kimwili, kihisia na kiakili. Kijana anaanza kujitafuta, kujenga utambulisho wake na kutaka kuhisi kuwa ana sauti katika maisha yake. Ndiyo maana amri nyingi, lawama na vitisho mara nyingi huzaa upinzani badala ya ushirikiano.

Swali muhimu kwa mzazi si "nitamlazimishaje afanye?" bali "nitamsaidiaje ajihamasishe mwenyewe?"

Njia ya kwanza ni kumpa kijana nafasi ya kuchagua ndani ya mipaka iliyo salama. Vijana huhamasika zaidi wanapohisi wanashirikishwa katika maamuzi yanayowahusu. Badala ya kusema, "Nenda kasome sasa hivi," mzazi anaweza kuuliza, "Mpango wako wa kusoma leo ni upi?" Au, "Unaona ni muda gani utakufaa kumaliza kazi hii?"

Maswali kama haya hayapunguzi mamlaka ya mzazi. Badala yake, yanamfundisha kijana kufikiri, kupanga na kuwajibika. Mzazi bado anaweka mipaka, lakini ndani ya mipaka hiyo kijana anapewa nafasi ya kutumia akili yake.

Njia ya pili ni kusikiliza kabla ya kuhukumu. Vijana wengi wanaoitwa wavivu au wasiojali huwa wanapambana na mambo ambayo wazazi hawajayaona. Wengine hawajui kupanga muda, wengine wanahisi kuzidiwa na majukumu, wengine wamepoteza kujiamini baada ya kushindwa mara kadhaa.

Badala ya kuuliza kwa hasira, "Kwa nini hujafanya kazi yako?" ni bora kuuliza kwa utulivu, "Ni nini kinakuzuia kufanya kazi hii?" Swali la kwanza linatafuta kosa; la pili linatafuta suluhisho. Kijana anayesikilizwa huwa na nafasi kubwa zaidi ya kufunguka na kushirikiana.

Njia ya tatu ni kusifu juhudi badala ya kipaji pekee. Maneno ya sifa yanaweza kujenga au kudhoofisha hamasa. Badala ya kusema tu, "Wewe ni mwerevu," mzazi anaweza kusema, "Nimeona ulivyofanya kazi kwa bidii," au "Nimefurahishwa na uvumilivu wako." Sifa ya aina hii humfundisha kijana kuwa mafanikio yanatokana na juhudi, uvumilivu na kujifunza, si kipaji pekee.

Ni muhimu pia kutambua mafanikio madogo. Wazazi wengi huona makosa haraka kuliko maendeleo. Kijana anayesikia kila siku kile alichokosea huanza kuamini kuwa hawezi kufanya vizuri. Lakini anapotambuliwa kwa hatua ndogo alizopiga, hujenga kujiamini na motisha ya kuendelea.

Njia ya nne ni kumruhusu ajifunze kutokana na makosa. Wazazi wengi hujaribu kuwaokoa watoto wao dhidi ya kila kosa, lakini kushindwa ni mwalimu muhimu. Kijana akisahau kazi ya shule na kukutana na matokeo yake, anaweza kujifunza zaidi kuliko angefundishwa kwa mihadhara mirefu.

Hii haimaanishi kumuacha peke yake. Inamaanisha kuwa karibu naye bila kufanya kazi kwa niaba yake. Mzazi anaweza kusema, "Najua umeumia kwa matokeo haya. Umejifunza nini? Unafikiri unaweza kufanya tofauti wakati mwingine?" Hapo kijana anajifunza kutatua matatizo badala ya kukimbia lawama.

Njia ya tano ni kutumia zawadi na mapumziko kwa busara. Zawadi si lazima ziwe fedha au vitu vya gharama kubwa. Inaweza kuwa dakika chache za kupumzika baada ya kazi, muda wa kufanya jambo analolipenda au nafasi ya kuchagua shughuli fulani ya familia. Hata hivyo, zawadi zisigeuke rushwa ya kila siku. Lengo ni kumsaidia aanze, si kumfundisha kuwa kila jukumu lina malipo.

Mwisho, mzazi anapaswa kuwa mkarimu lakini thabiti. Upole bila mipaka unaweza kulea uzembe; ukali bila upendo unaweza kuzaa uasi. Kijana anahitaji kujua kuwa anapendwa, lakini pia anawajibika.

Lengo la malezi si kumfanya kijana atii leo tu, bali kumwandaa kuwa mtu mzima anayejiongoza kesho. Kijana anayefundishwa kuchagua, kupanga, kujitathmini na kuwajibika huwa na nafasi kubwa ya kujenga hamasa ya ndani. Kwa hiyo, siri ya kumhamasisha kijana barobaro si kumdhibiti zaidi, bali kumwezesha zaidi.

**MAKALA**
**SAIKOLOJIA**

UKHTI FATIMA SS




# Kukubali kukosolewa ni alama ya ukomavu wa akili

**Katika maisha ya kila siku, watu wengi hupenda kusifiwa lakini wachache hupenda kukosolewa. Haijalishi ni mwanaume au mwanamke, mara nyingi mtu anapoelekezwa kosa fulani, hisia za kwanza huwa ni kujitetea, kukasirika au kuhisi amedharauliwa.**

**Hata hivyo, wataalamu wa saikolojia na maendeleo binafsi wanaeleza kuwa uwezo wa kupokea ushauri na ukosoaji wa kujenga ni moja ya alama muhimu za ukomavu wa akili na hisia. Mtu anayekubali kusahihishwa huwa na nafasi kubwa ya kujifunza, kukua na kuboresha mahusiano yake na watu wanaomzunguka.**

## Kukosolewa si sawa na kushambuliwa

Moja ya sababu zinazowafanya watu wengi wachukie kukosolewa ni kuchanganya ukosoaji na shambulio dhidi ya utu wao. Mtu anapoambiwa kuwa amekosea katika jambo fulani, hujisikia kana kwamba thamani yake yote kama binadamu imepingwa.

Kwa hakika, kuna tofauti kubwa kati ya kukosolewa na kudhalilishwa. Ukosoaji wa kujenga hulenga kurekebisha tabia, mtazamo au kitendo fulani. Kudhalilisha, kwa upande mwingine, hulenga kumuumiza au kumshusha mtu.

Mtu mwenye busara hujaribu kwanza kuchunguza ujumbe uliopo ndani ya maneno aliyosikia badala ya kuangalia namna tu yalivyosemwa.

## Wanaokujali mara nyingi ndio wanaokuelekeza

Katika mazingira mengi, watu huwa hawatumii muda wao kuzungumzia mambo ambayo hayawahusu. Mara nyingi mtu anapoona unaelekea kufanya kosa au una tabia inayoweza kukudhuru, huhisi wajibu wa kukueleza.

Bila shaka si kila ukosoaji ni sahihi. Wapo wanaokosoa kwa chuki, wivu au kutafuta mabishano. Hata hivyo, ukweli unabaki kuwa mara nyingi watu wanaokujali ndiyo wanaokuwa tayari kukueleza ukweli ambao wengine wanaogopa kuusema.

Ndiyo maana si busara kupuuza kila ushauri au ukosoaji kwa sababu tu haukupendeza kuusikia.

## Kukubali kusahihishwa ni alama ya ukomavu

Hakuna mwanadamu mkamilifu. Kila mmoja wetu ana mapungufu, makosa na maeneo yanayohitaji kuboreshwa.

Mtu aliyekomaa kiakili anakubali ukweli huu. Anajua kwamba anaweza kujifunza kutoka kwa wazazi wake, mwenzi wake, watoto wake, marafiki zake, wafanyakazi wenzake au hata watu walio chini yake kwa umri au cheo.

Badala ya kupinga kila anachoambiwa, hujiuliza kwanza: “Je, kuna ukweli wowote katika jambo hili?” Swali hilo pekee linaweza kufungua mlango wa maendeleo makubwa binafsi.

Kwa upande mwingine, mtu anayekataa kusahihishwa mara zote hujifungia mlango wa kujifunza. Huanza kuamini kwamba yeye ndiye anayejua kila kitu, hali ambayo mara nyingi husababisha makosa kurudiwa tena na tena.

## Ukimya si mara zote ni habari njema

Watu wengi hufurahi wanapoacha kukosolewa. Hata hivyo, ukimya si mara zote ni ishara ya kwamba kila kitu kiko sawa.

Wakati mwingine watu huacha kutoa ushauri au maoni kwa sababu wamechoka, wamekata tamaa au wameona hakuna anayesikiliza. Katika mazingira ya kazi, familia au urafiki, hali hii inaweza kuwa hatari zaidi kuliko ukosoaji wenyewe.

Mawasiliano ya wazi na uwezo wa kusahihishana kwa heshima ni miongoni mwa misingi ya mahusiano na taasisi zenye afya.

## Uislamu unahimiza nasaha

Katika Uislamu, kutoa na kupokea nasaha ni sehemu muhimu ya maisha ya Muislamu. Waumini wanahimizwa kusaidiana katika mema, kuamrishana yaliyo mema na kukatazana maovu kwa hekima na upole.

Hivyo, kupokea mawaidha kwa moyo wa kujifunza ni sifa inayopendwa. Vilevile anayetoa ushauri anatakiwa kufanya hivyo kwa heshima, busara na nia njema. Lengo la nasaha si kumshinda mtu katika mabishano, bali kumsaidia awe bora zaidi.

Kwa hiyo, kukosolewa si jambo linalopendeza kila wakati, lakini mara nyingi ndilo daraja la kuelekea kwenye mabadiliko na maendeleo. Mwanaume au mwanamke mwenye ukomavu wa akili hasikii maneno pekee; hutafuta kuelewa ujumbe uliopo nyuma ya maneno hayo.